

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Tatu - Tarehe 28 Januari, 2010**

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Muuliza swali wa kwanza ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu nafikiri unakumbuka tarehe 5 Novemba, 2009 Dr. Aman Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, walikutana na hatimaye chama cha CUF kikamtambua na kuitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni nini *position* ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya maridhiano haya?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, wako watu watatu au wanne wakisimama najua ni yaleyale tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama nitakuwa na jibu zuri sana, lakini niseme kwamba tunao mfumo mzuri sana wa namna ya kufanya maamuzi makubwa kama haya. Sasa ni kweli jambo hili limetokea pale Zanzibar lakini mimi imani yangu ni kwamba katika kutekeleza ule mfumo wa namna ya kufanya maamuzi yafikie ukomo wake naamini ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwa kutumia Kamati maalumu ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Zanzibar bila shaka jambo hili litakuwa tayari limeshazungumzwa, ndiyo imani yangu mimi. (*Makofi*)

Naamini vilevile kwamba baada ya hapo hatua itakayofuata ni kulileta jambo hili sasa *formally* kwenye Chama cha Mapinduzi kupitia Kamati Kuu pamoja na Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa hiyo, kama ni jibu sahihi juu ya nini mtazamo wa Serikali itakuwa ni baada ya chama kuwa kimefanya maamuzi na kuielekeza Serikali ifanye nini katika jambo hili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naamini kabisa tutakapofika hatua hiyo ukiniuliza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed mimi nitakuambia kimesemwa nini kama Serikali lakini ukiniuliza tu kwamba maoni yako wewe kama Pinda unasema nini na mimi ningesema vilevile kwamba kama Watanzania wengi wanavyofikiria kwamba ni jambo jema na mimi nafikiri ni jambo jema kwa maana tungependa Zanzibar ikawa na yenyewe ni eneo la utulivu na amani badala ya kukaa mnavutanavutana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati yuko Egypt baada ya kupata taarifa hizi alitoa salamu na kuunga mkono hatua hii na hatimaye katika hotuba zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na ile ya mwisho wa mwezi vilevile aliliunga mkono. Je, haionekani hiyo tayari ni *position* ya Serikali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nchi yoyote mnayokuwa na Rais mwenye madaraka wanamuita *Executive President* ye ye kusema kweli ndiye anaweza kusema jambo lolote juu ya nchi yake. Kwa hiyo, ye ye alikuwa analisema kama kiongozi wa nchi hii na mimi napenda niamini kwa dhati kwamba ni imani yake kwamba jambo hili lina ubora na ukiniuliza mimi nitasema pengine ni kiashiria kizuri kwamba hata likija kwenye chama na pengine kwenye Serikali tunadhani wote tutakwenda na msimamo wa namna hiyo. Mimi nadhani ndiyo fikra zangu zinakonituma.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa, baadhi ya migogoro ya mipaka hapa nchini inachukua muda mrefu sana kupatiwa ufumbuzi na kuwaacha wananchi wa maeneo haya wakishindwa kuaminiana na kuishi kwa uhasama na kwa kufanya hivi basi migogoro inasababisha kukwama kwa huduma za maendeleo, na kwa kuwa mgogoro wa mpaka wa Manyoni na Sikunge Mheshimiwa Waziri Mkuu unaufahamu vizuri tangu ukiwa Naibu Waziri halafu ukawa Waziri halafu leo Waziri Mkuu. Mgogoro huu umedumu takribani miaka 20, naomba nikuulize Serikali inasema nini juu ya kuamua sasa na kutoa maamuzi ambayo yatahitimisha mgogoro huu uliodumu kwa muda mrefu sana?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi Bungeni humu nina miaka kidogo sana sijafika hata hiyo miaka 15, lakini anachosema ni kwamba inaonekana ni muda mrefu wamekuwa wakivutana, ni kweli kwamba nimekuja nikalikuta kama Naibu Waziri na nilikwenda pale tukafanya juhudzi za awali na bado naamini litatafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini matatizo haya ya mipaka ndani ya nchi kati ya kijiji na kijiji, kata na kata au tarafa na tarafa au Wilaya na Wilaya, mkoa na mkoa katika mazingira ya kawaida halipaswi kuwa jambo kubwa kiasi cha kutufikisha mahali tukaanza kuhatarisha hata usalama wa wananchi, hata kidogo!

Tatizo ninaloliona tu ni kwamba mara nyingi Viongozi wa kisiasa ndiyo tunaolikuza sana hili jambo kwa sababu upande mmoja uking'ang'ania msimamo fulani hautaki kuona kwamba pengine kinachohitajika hapa ni suluhi tena ni suluhi ya haraka.

Sasa kwa swali la Mheshimiwa Nkumba ni kweli kwamba kuna mgogoro kati ya Manyoni na Sikunge katika Kijiji kimoja cha Kalangali, suala pale ni kama Kalangali iko Sikunge ama iko Manyoni. Kijiji cha Kalangali kinapata huduma zake zote Manyoni kwa sababu kiko karibu zaidi na Wilaya ya Manyoni, na kiko mbali na Makao Makuu ya Sikunge. Sasa kwa maana ya mpaka inaonekana Kalangali iko Sikunge lakini kwa maana ya hali ya uhalisia ulivyo kwa kweli Kalangali iko Manyoni kwa madhumuni yote, kinachohitajika hapa ni pande hizi mbili kukaa na kukubaliana kwamba hawa wana Kalangali acheni waendelee kuhudumiwa na Manyoni, acheni waendelee kupiga kura Manyoni kwa sababu mipaka haiwezi kuwa ndiyo ukuta kati ya Wilaya ya Sikunge na Wilaya ya Manyoni.

Sasa nimemwambia Mheshimiwa Nkumba na wenzake kwamba kaeni chini mkiridhiana hili mkaelewana hivyo halina tatizo kwanza sisi wengine wote tutanyamaza kwa sababu litakuwa limekwisha, lakini kama mtaamua kwamba Kalangali lazima iende Sikunge na wenyewe wanasema Sikunge hakuna huduma, tuko mbali mno sisi tutaendelea kuwa Manyoni hamtalimaliza hata kidogo.

Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Nkumba kwamba kaeni pande zote mbili. Mimi ukiniuliza sasa ninaona suluhi nzuri kabisa ni kwenda kule ambako kimsingi huduma zinapatikana acheni wafuate huduma zao pale. Suala la mpaka ni kwenye makaratasi na kwa madhumuni ya utawala ikibidi tutamuomba Rais akiridhia kwamba tupindishe mpaka sasa tutafanya lakini kwa madhumuni ya zoezi hili mimi nadhani hiyo ndiyo ingekuwa njia sahihi na ya kweli.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama unavyojuwa kuwa Zanzibar kwa maana ya Unguja iko gizani toka tarehe 10 Desemba 2009 kutokana na kukosa umeme uliosababishwa na kuharibika kwa chombo fulani kilichoko Fumba Zanzibar kinachopokea umeme na vilevile kutokana na uchakavu wa waya na mitambo. Hali hii ya giza totoro inatarajiwa kuendelea hadi tarehe 20 Februari mwaka huu, kwa hiyo muda huu wa siku 40 hadi sasa umeathiri sana shughuli zote za kijamii na kimaendeleo kiasi cha kutikisa uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waswahili wanasema udugu ni kufaana si kufanana, kwa mantiki hiyo basi je Serikali ya Muungano wa Tanzania ina mpango gani au imetumia juhudii gani za kuondoa tatizo hili ambalo linajirudia mara kwa mara?

**WAZIRI MKUU:** Udugu ni kufaana na siyo kufanana, kwa sababu Mheshimiwa Khamis kila mara ananiuliza maswali magumumagumu hivyo wala hakuna udugu basi tu tuvumiliane. (*Kicheko*)

Lakini nataka niseme kwamba wote lazima tukubaliane kwamba ni tatizo kubwa na lazima tuunge mkono juhudhi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwa kweli tuungane na Wazanzibar wote kusikitishwa na tukio ambalo kwa kweli limeathiri sana huduma nyingi sana pale Unguja.

Niliandikiwa barua na Waziri Kiongozi kutoka Zanzibar na tukaipokea, na tulichofanya tukaanza kuishughulikia kwa maana ya kujaribu kuona katika kipindi hiki kigumu maana sasa tunajua wanajaribu kutumia kila mbinu yaani kutumia pesa nyingi kugharamia mafuta hasa kwa ajili ya kuendesha jenereta ndogondogo za hapa na pale na kwa kweli inawagharimu pesa nyingi. Kwa hiyo, na sisi tunalitazama. Serikalini limeshafika mpaka kwa Waziri wa Fedha tuone mchango wowote ambao tunaweza tukawa nao kusaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kujaribu kupunguza mzigo ambao sasa wameubeba katika mazingira ambayo hawakuyategemea.

Lakini ni kweli kwamba nyaya zile zimechakaa, muda wake wa kuishi kusema kweli umepita. Ni kitu kinataka marekebisho makubwa sana lakini tuko pamoja katika tatizo hili na mimi nina hakika baada ya muda si mrefu sana tutakuwa tumeshatoa kile ambacho tunafikiri tutaweza.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante kwa majibu yako. Lakini imethibitishwa kwamba *ZECO* Shirika la Umeme Zanzibar limepata hasara karibu ya Shilingi bilioni mbili (2) kutohana na kutokusanya haya mapato kwa hiyo imeathirika sana kiuchumi na kwa mantiki ileile ya udugu ni kufaana, kuna *TANESCO* hapa ambayo *ZECO* ni wateja wakubwa wa *TANESCO* lakini vilevile ni ndugu zao, kwa nini basi *TANESCO* isiwasaki ZECO ili kujikwamua hapo walipo kwa sababu wako katika hali mbaya ya mahututi.

**WAZIRI MKUU:** *TANESCO* isiwasaki nini? Maana mimi nimedhani kwamba hili jambo lilipoletwa kwangu ni kwa sababu walitaka kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano tuone namna tunavyoweza kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, mimi nadhani ni la Serikali na *TANESCO* ni chombo tu cha Serikali hata kama kutakuwa na namna sisi ndiyo tutakielekeza nini wafanye.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki sana katika kupigania uhuru katika Bara la Afrika, sasa nauliza kwa nini Wafaransa bado wanang'ang'ania moja ya visiwa vya Comoro na Comoro yenye ni nchi huru, wataondoka lini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kipindi hiki nakiogopa kweli, sina hakika kumbukumbu zangu kama zitanisaidia sana kwenye historia ya visiwa vya Comoro lakini niseme tu kwa kifupi kwamba tuna visiwa kama vinne pale, na katika kuamua juu ya kujikwamua kutoka kwenye ukoloni wa Mfaransa kama kawaida walipiga kura za maoni kwa hiyo nadhani visiwa vitatu wao wakaamua kujitenga na kuwa huru na hawa visiwa hivi vitatu na leo viko huru na kwa kweli vinaendesha taratibu zake pale

vizuri na ule urais wao ni wa kuzunguka. Kisiwa kimoja chenyewe kupitia kura hizo kiliamua kubaki ni sehemu ya Mfaransa au sehemu ya Ufaransa, sasa hayo ndiyo maamuzi yaliyofanyika ni matakwa ya wananchi wa Kisiwa hicho hatuwezi sisi tukasema kwa nini hamkufanya vinginevyo labda polepole ni kuendelea kuwashawishi au wenyewe watafika mahali wataona kwamba pengine wakati umefika wa kuweza sasa kuamua kuanza kujitegemea kama wenzao. Kwa hiyo, nadhani ilikuwa ni uamuzi wa wananchi tu sidhani kama kuna kitu kingine.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi ni ukoloni, ndiyo jambo. Kura zilipokuwa zinapigwa Wafaransa walifanya kampeni kwa sababu kile kisiwa wanakipa huduma kuliko visiwa vingine vyote kwa hiyo Ufaransa wanatoa rushwa wakati wa kampeni ili waendelee kutawala kile kisiwa. Je, AU haiwezi kuweka mguu katika jambo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi naogopa pengine kuishtaki Serikali hiyo kwa rushwa kwa sababu sina hakika kama tuna ushahidi wa kutosha kiasi hicho lakini mimi nirudie niseme kwamba kupanga ni kuchagua, kisiwa kile waliamua kwamba wanataka kuendelea kuwa ni sehemu ya nchi ya Ufaransa, kwa sababu kama ni *influence* hata visiwa vingine hivyo vingeweza *influenced* vilevile lakini visiwa hivyo vingine vilisema hapana. Mimi nafikiri katika mazingira haya tuheshimu maamuzi ya wananchi wa Kisiwa hicho mpaka watakapoona vinginevyo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa leo tayari yamekwisha na ni fafanue tu kwamba utaratibu wa maswali yawe kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au maswali ya kawaida yanapokwisha maswali, basi! Maana yake wengine wanaweza kusema kwa nini Spika hakuruhusu muda ulikuwa bado, hapana!

Kwa mfano katika orodha ya shughuli maswali yakiisha kabla basi tunaendelea na shughuli inayofuata.

La pili, tumekubaliana baada ya kupima uzoefu pale ofisini kwamba wale wanaojitokeza takribani kila wiki kama Mheshimiwa Salim Hemed Khamis sasa nao basi, kwenye mkutano mmoja watapata fursa ya swali moja lakini hawawezi kuwa kila Alhamisi wanajitokeza kwa kuwa ni wepesi tu kuja pale ofisi na kujiandikisha. Kwa hiyo, kwa tahadhari hiyo naomba mzingatie kwa Alhamisi ijayo kama Ndugu yetu Mheshimiwa Salim hodari sana lakini ajue hilo alilouliza leo ndiyo la mwisho kwa mkutano huu wa kumi na nane (18). (Kicheko)

Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana.

#### **MASWALI YA KAWAIDA**

### **Utumikishwaji wa Watoto Wadogo**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa utumikishwaji wa watoto ni kosa la jinai kwani kunawakosesha hazi zao za msingi kama vile elimu, fursa ya kucheza, kukosa uhuru wa kuishi na jamii nk, na kwa kuwa jumla ya watoto 2,180,000 wako katika utumikishwaji:-

Je, ni Mikoa gani inayoongoza kwa utumikishwaji wa watoto wenyе umri wa miaka Saba mpaka Kumi na Saba (7-17 ) hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa utumikishwaji wa watoto kuanzia umri wa miaka 7-17 ni tatizo kubwa hapa nchini. Hali hii inawanyima watoto haki zao za msingi zikiwemo kukosa elimu, kucheza, kulindwa na kutunzwa na wazazi pamoja na kuwa na afya bora.

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizonazo hazonyesi tatizo hili kimkoa au kiwilaya kwa nchi nzima, bali zinaonesha kisekta au maeneo ya kiuchumi. Hii inathibitishwa na tafiti zinazofanyika kila baada ya miaka mitano kuangalia ukubwa wa tatizo hili hapa nchini (*Intergraded Labour Survey*) na utafiti wa mwisho ulifanyika mwaka 2006. matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa 20.7% ya watoto wa umri huo wanatumikishwa katika kazi yenye madhara. Sekta zilizobainika kuongoza katika utumikishwaji wa watoto ni sekta za kilimo, uvuvi, madini na utumishi wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, tunao mfano wa utafiti mdogo uliofanywa na Taasisi ya REPOA kwa ushirikiano na ILO mwaka 2007/08 katika sekta ya uvuvi kwenye wilaya za Lindi, Kilwa, Ilemela, Unguja Kaskazini A na Micheweni. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa, Kilwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wanaotumikishwa kwenye uvuvi, ikiwa na idadi ya watoto 2,063 ikifuatiwa na Wilaya ya Lindi watoto 976, Unguja Kaskazini A watoto 745, Ilemela watoto 530 na Micheweni watoto 340.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yake mazuri lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Je, baada ya kupitishwa Sheria hii mpya juzi je, Serikali imejipanga vipi juu ya kupunguza idadi ya watoto wanaonyanyaswa katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwanzoni tulikuwa tunashindwa kutetea haki za watoto ipasavyo kwa sababu tulikuwa hatuna Sheria ambayo ilikuwa inatoa mwongozo kamili.

Baada ya hii Sheria kupitishwa na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wizara yangu itatengeneza Kanuni na itahakikisha kwamba sasa tunaanza kutoa mafunzo kwa wale watekelezaji wa kuhimiza kwamba Sheria na haki za watoto zinakuwa zinafuatwa na baada ya hapo ni kwamba pale ambapo sasa tulikuwa tunashindwa kumkamata mzazi kwa kushindwa kumleta mtoto, pale ambapo tulikuwa tunashindwa kumkamata mtu anayetumikisha watoto sasa Sheria inatupa meno kupitia Idara zinazohusika maana yake Wizara ya Sheria na Katiba pamoja na Uongozi katika Serikali za Mitaa pamoja na Walimu mashulen ambao tunaamini kwamba watatusaidia sna katika kufuatilia sasa na kuhimiza kwamba hii Sheria inafuatwa. (Makofi)

**MHE. DR. ZAYNAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa hivi sasa watoto wakimaliza darasa la saba wanamaliza wakiwa na miaka 14 na kuna watoto ambao hawakufaulu wazazi wao hawna uwezo kabisa wanatafuta kazi wakiachiwa wasichana watapata mimba na wavulana wataingia kwenye bangi matokeo yake wanaajiriwa majumbani.

Je, Serikali ina utaratibu gani kuwasaidia watoto hawa?

**SPIKA:** Tunaomba ufundi mrekebishe hali ya taa imeanza kuwa giza humu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Zaynab Gama kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna watoto ambao sasa kwa sababu tumekuwa na shule nyingi wanafaulu watoto wengi lakini kwa bahati baya kuna watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuweza kuwalipia waendelee na masomo ya sekondari ambayo sasa hivi tunakukwa na intake kubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kwamba ushirikiano kati ya wizara zinazohusika mimi ninaamini kwamba Wizara ya Elimu imesikia hilo na Wizara ya TAMUSEMI ambayo sasa hivi ndiyo imepewa jukumu la kufanya hivyo tutawasiliana nao na ninaamini kwamba tunaweza tukapata jibu. Lakini mimi naomba nitoe wito kwa Serikali za vijiji, kwenye kila Serikali ya kijiji kuna Kamati ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kwa hiyo mimi ninaomba uongozi wa Halmashauri uhakikishe kwamba unawajengea uwezo hizi kamati ziwezi kuangalia namna ya kuwasaidia hao

watoto ambao ninaamini kwamba wako chini ya uongozi wao na wao ndiyo watahakikisha kwamba hao watoto wanasona shule.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo hawa watoto wanatumikishwani maeneo ambayo hakuna shule za msingi ama hakuna shule za kutosha za sekondari. Kama Serikali ingeweza ikafanya utafiti ikajua kwamba ni vijiji vingapi ambavyo shule za msingi ama shule za sekondari ziko mbali sana na maeneo wanayotoka hawa watoto na kuhakikisha kwamba zinakuwepo shule karibu za kutosha za msingi.....

**SPIKA:** Lenga kwenye swali tafadhali, maelezo ni mrefu mno!

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Naomba niulize, je mmeefanya utafiti wa kutosha wa kuona kwamba maeneo haya ambayo watoto wanatumikishwa ni yale ambayo watoto hawana nafasi ya kwenda shule ama kwa wazazi wao kutokuwapeleka ama shule kutokuwepo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO :**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpaka sasa hivi hatujaweza kufanya tafiti kijiografia kujua kwamba haya maeneo ambayo watoto wanatoka kwenda kufanya kazi ni wapi, lakini kwa takwimu ambazo zipo na kwa shughuli ambayo imefanyika ni kwamba hao watoto ambao wako kwenye machimbo ya madini au mashamba wote wanatoka kwenye vijiji ambavyo kuna shule.

Sasa hawa watoto wametoka kule kwa sababu nyingine mbalimbali na ninaomba niseme kwamba sababu kubwa inayofanya watoto wanakwenda kutumikishwa siku hizi ni kukosa wazazi kwa ajili ya janga la UKIMWI na ya pili ni kwamba wazazi wamekura ni fukara wanawatuma watoto wakafanye kazi wachangie katika kipato cha familia. Sasa hapo ndiyo nasema kwamba tatizo siyo shule tatizo sasa hivi ni ufuatiliaji na reinforcement ya Sheria mpya ya mtoto. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sna Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa Wizara hiyohiyo linaulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar Viti Maalum.

Na. 30

### **Kuanzisha Tawi la Benki ya Wanawake Zanzibar**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha Benki ya Wanawake Tanzania, mpango utakaowakomboa Wanawake wengi katika kujiwekea fedha na kupatiwa mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza kibiashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua tawi la Benki hiyo Tanzania Zanzibar ili Wanawake wa Zanzibar nao waweze kunufaika na huduma zitolewazo na benki hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Fakar Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kama Kauli Mbiu ya Benki inavyosema “Benki pekee kwa wote” Benki ya Wanawake Tanzania ilifunguliwa kwa lengo la kuwahudumia Wanawake na Wanaume wote Tanzania. Kwa sasa, Benki hii ina tawi moja lililopo katika mtaa wa Mkwepu, Jijini Dar es Salaam. Mipango ya baadae ya Benki hii ni kufungua matawi kote nchini ikiwemo Zanzibar kwa kadri itakavyoendelea kukua na kijiimarisha kimtaji.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi wote, Wanawake kwa Wanaume, Taasisi mbalimbali zikiwemo za kidini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Halmashauri za Wilaya na wadau wengine wa maendeleo kufungua akaunti na kununua hisa katika Benki ya Wanawake ili kuiwezesha Benki hii kukua haraka na hivyo kujenga uwezo wa kufungua matawi mengine kote nchini.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki hii ya Wanawake Tanzania, lakini swali langu ni hili;

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameongea kwamba, itakuwepo mipango ya baadae ya kuanzisha benki hii Zanzibar na mikoani kote ama nchini kote, lakini kwa sasa ni bado na baadae hatujui ni lini angesema labda mwaka fulani hapo ndiyo ningefurahi lakini amesema baadae, baadae hatujui ni lini;

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha wakala wao Zanzibar na Mikoani ili kuwapatia mahitaji Wanawake wa Tanzania kutokana na benki hii?

Mheshimiwa Spika, la pili ninaongea kwamba, wakati wa kuanzisha benki hii hapa Tanzania, Serikali ilihamasisha wananchi kununua hisa, kuwekeza fedha katika benki hii ya Wanawake na sisi tukajitokeza kuchangia lakini mpaka sasa hatujapata vitambulisho, sijui Serikali ina mpango gani wa kutupatia angalau vitambulisho tujulikane kama tumechangia katika benki hii, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Faida Mohammed Fakar, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nishukuru kwa niaba ya Serikali kwa pongozi alizozitoa, kwa kweli Serikali inastahili pongozi.

Mheshimiwa Spika, swal la pili; wazo au ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kutafuta wakala kule visiwani Zanzibar kusudi wanawake wa Zanzibar waweze kupata na wao *accesses* ya kupata huduma za hii benki ni wazo zuri sana naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaangalia tutaanza kulifanyia utafiti lakini kusema muda *specific* ni ngumu kidogo kwa sababu ndiyo benki inaanza kujiwekea mitandao, lakini hili ni suala ambalo tutalifanyia utafiti haraka iwezekanavyo ili tuone uwezekano wa kuwa na wakala kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, swal la pili kuhusu vitambulisho; ni kweli Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilihamasisha wadau wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kununua hisa katika benki hii. Hii benki ndiyo imefungua milango yake, inaanza kutengeneza mitandao yake ya kazi na inaanza sasa hivi kutengeneza *certificates* za wale ambao wamenunua hisa na naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, haitachukua muda mrefu kila mmoja ambaye amenunua hisa katika benki yetu atakuwa amepata kitambulisho.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, Mungu akubariki. Mimi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nimeshangaa kidogo pale alipotoa wito kwa wilaya zote na halmashauri zote kwamba, wafungue akaunti kwenye benki hii ya Wanawake ambapo tunajua Makao Makuu yake yako Dar es Salaam, sasa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie; Wilaya na Halmashauri zote watafungua akaunti kwa kufuata Dar es salaam ama vipi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimesema kwamba, benki yetu ina makao makuu Dar es Salaam na kwa sasa hivi tuna tawi moja tu lakini katika kutengeneza mchakato wa kuwezesha Wanawake tuliweka kifungu ambacho nafikiri ni asilimia 25 au asilimia 20 , tumetenga kwa ajili ya halmashauri zote nchini wanunue hisa na wakinunua hisa kwenye benki yetu si kufungua tu akaunti, wakiamua kufunga akaunti, kufungua akaunti vyema lakini naomba kusema kwamba, msisitizo wetu ni kwamba wanunue hisa ili waweze kukopa pesa ambazo zitaingia kwenye ule mfuko wao wa kuwapa Wanawake mikopo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nafikiri kwamba, hilo ni jambo zuri hata tutakopofikia sasa kwenda kufungua matawi wilayani basi tutaangalia ni nani ambaye amekuwa ni mdau mkubwa kuliko wadau wengine ndiyo tutaanza kwenda kule kwa sababu hapo ndipo ambapo tutakuwa na wateja ambao wataleta faida kwetu kwa sababu sisi ni benki ya biashara tutahakikisha kwamba, ile benki inazalisha kusudi Wanawake waweze kupata mikopo.

Na. 31

### **Mpango wa Mabehewa ya Ghorofa kwa Treni ya Reli ya Kati**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mipango inayoandaliwa na Serikali kuboresha usafiri wa treni kwa Reli ya Kati inayoanzia Dar es Salaam kwenda Tabora hadi Kigoma na Mwanza, na pia kuelekea Moshi na Arusha; na kwa kuwa, mipango hiyo ni pamoja na kupanua geji ili iwe pana zaidi na vilevile kuongeza huduma mpya ya reli kutoka Isaka hadi Kigali (Rwanda) na Bunjumbura (Burundi); na kwa kuwa nchi za Afrika Mashariki zimeamua kuanzisha soko la pamoja (*East African Common Market*):-

- (a) Je, serikali katika mipango yake imefikiria kuingiza mabehewa ya ghorofa (double decker coaches) ili kuongeza nafasi nyingi zaidi kwa abiria kama nchini nyingi duniani zinavyofanya?
- (b) Kama jibu ni ndiyo. Je, utaratibu huo utaanishwa lini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inaandaa mipango ya kuboresha usafiri wa reli kwa kupanua geji kutoka mm 1000 (metre gauge) hadi mm 1435 (standard gauge). Serikali imekwishafanya upembuzi yakinifu wa kuboresha reli ya kati kuanzia Dar es Salaam hadi Isaka na kujenga reli mpya ya Isaka -Kigali na kutoka Kigeza-Gitega -Musongati nchini Burundi ili iwe katika *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upembuzi yakinifu uliofanywa na Mshauri Mwelekezi, huduma itakayotolewa ni ya kubebea kontena kwa mtingo wa *double stack* na sio mabehewa ya ghorofa. Hata hivyo kwa kuwa reli hiyo itajengwa ikiwa na uwezo mkubwa zaidi wa kubebea abiria na shehena na mwendo kasi wa kilomita 120 kwa saa, abiria wengi wataweza kusafirishwa kwa muda mfupi na kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata na ambayo inashughulikiwa na nchi zetu tatu za Burundi, Rwanda na Tanzania ni kutafuta fedha kwa mfumo wa kushirikisha sekta binafsi na umma (PPP) ili kufanya usanifu wa kina na ujenzi.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nilitaka pia kufahamu katika kuboresha reli hizi, reli ambazo ziko sasa hivi kama reli ya kati ya mwanza na kadhalika, na reli ambazo zitakuja kujengwa kwenda Rwanda na Burundi;

Je, Serikali imekwisha fanya au kufikiria mpango wowote wa kukarabati stesheni zote zilizopo kandokando ya reli hizo na pia stesheni ambazo zitajengwa katika reli mpya, vilevile wakizingatia katika stesheni hizo kujenga *platform* za zege ili kuwezesha watu kama Walemvu, Wazee na Wanawake Wajawazito waweze kupanda kwa urahisi? (*Makofifi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swalila nyongeza la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, kama ifuatavyo;

Katika mpango wa ujenzi wa reli yetu ya kati kwa ushirkiano pamoja na nchi za Rwanda na Burundi, makubaliano ya kufanyakazi hiyo tumeyasaini mwezi wa Pili mwaka jana 2009 Mjini Arusha na kwamba, reli hii ni mpya kipande cha Isaka hadi Kigali na kuanzia Kigeza nchini Tanzania kupitia Gitega Burundi mpaka Musongati ni kama sehemu moja, lakini sehemu ya pili ni upanuzi wa reli yetu ya kati kuanzia Dar es Salaam bandarini mpaka Isaka.

Mheshimiwa Spika, ujenzi huu wa reli mpya ni kwamba, utakuwa na vipimo vipyta kama alivyouliza Mheshimiwa kwamba, inatoka kwenye reli finyu ama *metre gauge* kwenda *standard gauge* ambayo ni upana mkubwa zaidi, kwa hivyo vipimo vyake vitakuwa ni tofauti, reli itakuwa tofauti, stesheni zitakuwa tofauti na itabidi zijengwe upya kwa sababu reli hizi kufuatana na *design* ambayo itawekwa ama treni itakuwa na urefu wa Mita Mia Nane (800) ama urefu wa mita Elfu Mbili ( 2000) kufuatana na *design* ya mwisho ambayo itakubalika, mita 2000 maanake ni treni ya urefu wa Kilomita Mbili haitoweza kuhudumiwa na *platforms* hizi ambazo ziko hivi sasa, kwa hivyo ujenzi huu ni mpya kabisa na thabiti kwa sababu mpaka sasa serikali tatu kwa ujumla zimeishatumia jumla ya shilingi bilioni Tano na milioni Mia mbili (5,200,000,000) kwa ajili ya upembusi yakinifu, tunaenda kwenye *stage* ya pili na kwa maana hiyo ni kwamba, tunaenda kwenye usanifu kwa ajili ya ujenzi.

Wazo la kuwa na platforms ambazo zitakidhi mahitaji ya ndugu zetu walemvu ni wazo zuri namimi nitahakikisha kwamba, wakati wa *design* tunalifikisha hili kwa wenzenetu watakao *design* ili liweze kufanyiwa kazi vizuri.

**SPIKA:** Labda niruhusu sasa mawili Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Jirani yangu nimemsahau tena, ahsante.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi namimi kwa sababu ni mdaa wa kutumia reli ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza. Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba, wanarekebisha reli hii kuleta treni zenye mwendo wa kasi, namimi ninavyofahamu treni huwa inaenda kwa kasi sana, sasa

hii kasi ni ya kiasi gani naona itatutisha sana sisi tunaotumia huu usafiri wa treni kwenda Mwanza, naomba anifafanulie hii kasi itakuwa kasi ya kiasi gani?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo; reli sasa hivi inatembea kwa mwendo mdogo sana, wastani wa Kilomita Thelathini na Tano kwa saa (35Kph) ni mwendo ambao ni sawasawa na konokono, unatupa matatizo makubwa katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu na hakuna reli katika dunia hii sasa hivi ambayo inaenda kwa mwendo wa aina hiyo kwa hivyo tunapokwenda sasa kuboresha reli hii maanake tunakwenda kufuatana na taratibu na teknolojia ya hivi sasa, *design* tunayotegemea kuwa nayo ni ya treni ambayo itaweza kwenda kwa *speed* ya Mia na Ishirini (120Kph) sio kubwa sana Mheshimiwa Nyawazwa, kwa sababu juzi China wamezindua treni ambayo inatembea kwa Kilomita Mia Tatu na Hamsini kwa saa (350 Kph) mara Kumi ya Speed ambayo reli yetu sasa hivi inafanya.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujafika huko tunakotaka kwenda kuwa na treni za kwenda kasi ya kilomita Mia Moja na Ishirini kwa sasa (120 Kph) gari moshi ambazo zinatumika sasa hivi hasa mabehewa ya abiria yako katika hali mbaya kwa maana ya uchakavu, lakini achilia mbali uchakavu na kwa sababu yanafanyakazi na yanabeba abiria hayatunzwi, yako katika hali mbaya sana kiafya. Nimesafiri na gari moshi mwezi wa Kumi na Mbili na Januari mwaka huu na hususani gari ya kwenda Mpanda katika mabehewa ya daraja la kwanza na la pili; kuna kunguni, kuna mende, kuna panya jambo hili linahitaji pia wafadhili waje watusaidie, Serikali inaelekeza nini kuhusu kuondoa adha hizi kwa wasafiri wanaotumia mabehewa hayo? (Makofi)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swal moja la nyongeza la Mheshimiwa Arfi kama ifuatavyo; Kwanza kabisa nikiri kuwa tuna upungufu wa vifaa katika reli yetu hivi sasa, tuna upungufu wa vichwa vyta treni na tuna upungufu wa mabehewa.

Mheshimiwa Arfi amepanda treni ile mwezi wa Kumi na Mbili kutoka Mpanda, mimi nilikuwa Mpanda na kuingia kwenye mabehewa yale mwezi wa Kumi na Moja mwishoni, tatizo la Mpanda kama kwenye maeneo mengine kwa treni hii ni kwamba, vichwa pale havitoshi na mabehewa hayatoshi lakini Serikali inalitambua hilo, inalifanya mkakati kwa ngazi yake peke yake ukiacha hii ya ujenzi wa reli mpya. Treni ya Mpanda -Tabora haijaacha safari hata wakati mmoja, nampa hongera sana *Station Master* wa treni ile ya Mpanda- Tabora anafanya kazi nzuri sana na ninampa pongezi nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini treni hiyo pia ni safi haina panya wala mende wala kunguni nimeingia mimi mwenyewe ndani ya treni ile pamoja na wataalamu wangu, kwa

sababu lazima niseme kitu kile ambacho nimekiona kwa macho yangu, nilikuwepo bila taarifa nimeingia ndani ya treni bila taarifa, nimekaa na wasafiri ndani ya treni ile na picha zimetoka na kwenye taarifa imeonekana, hili siyo la kweli Mheshimiwa Spika. (Makofi)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, hizi kauli zote mbili ni nzito, ile ya Mheshimiwa Arfi na Mheshimiwa Waziri; Je, Mheshimiwa Waziri atakubali tufanye utafiti wa pamoja ili kuhakikisha ipi kati ya kauli hizi iliyokuwa ni sahihi? (Makofi)

**SPIKA:** Utafiti wa pamoja sijui mtafanyaje ili kupata ukweli kwa sababu inaweza ikatokezea katika maandalizi ya utafiti baadhi yenu mkapeleka abiria ambaao tayari wamebeba kunguni kwa hiyo itakuwa vigumu sana sasa kujua kama wadudu hawa wametoka ndani ya treni ama abiria wamewaleta, kwa hiyo naona tuendelee Waheshimiwa. (Kicheko)

Swali linifuata Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, linaulizwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga.

Na. 32

### **Waanzilishi wa Vituo vya Watoto Yatima Kupewa Masharti**

**MHE. LUCY THOMAS MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa vituo vingi vya kulelea watoto yatima au wanaoishi katika mazingira magumu vimekuwa katika hali duni hasa kutokana na wengi wa waanzilishi kuvifungua kwa malengo ya kujinufaisha wenyewe.

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa vituo vya aina hiyo?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kuweka masharti maalum kwa watu wanaofungua vituo hivyo?

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, makao ya malezi ya watoto yamekuwa yakifunguliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Makao ya watoto Na. 4 ya mwaka 1968 pamoja na Kanuni zake. Hata hivyo kumekuwa na baadhi ya makao ambayo yamekuwa

yakifunguliwa bila kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni tajwa hapo juu. Mengi ya makao haya ndiyo yaliyo katika hali duni na hayatoi huduma stahiki kwa watoto wanaolelewa katika makao hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, Idara ya Ustawi wa Jamii hufanya ufuatiliaji wa makao yote ya malezi ya watoto na inapobainika kwamba kuna makao yenyé mapungufu yanayoweza kurekebishika wahusika huelekezwa masharti ya kisheria ili makao husika yaweze kusajiliwa. Aidha, kwa makao ambayo yana mapungufu yaliyokithiri hufungiwa kutoa huduma. Vilevile kila tunapopata taarifa ya kufunguliwa kwa makao ya malezi ya watoto kinyume cha sheria, watalaan wetu huenda kufanya ukaguzi ili kuona kama yana sifa zinazokubalika kwa mujibu wa sheria. Pale ambapo inathibitika kwamba makao yaliyofunguliwa hayajakidhi masharti ya kisheria hufungiwa kutoa huduma.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu makao ya malezi ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi yamekuwa yakianzishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa sheria ya makao ya watoto Na. 4 ya mwaka 1968 pamoja na kanuni zake. Sheria hii sasa imefutwa kwa sheria ya mtoto na. 21 ya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine, inatoa taratibu mpya zitakazodhibiti uanzishaji holela wa makao ya watoto.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyyoatoa.

Mheshimiwa Spika, vituo hivi vinavyolea watoto yatima viko katika makundi na tofauti za aina mbalimbali; viko vituo ambavyo viko katika maeneo ya mijini, viko vituo katika maeneo ya vijijini, viko vingine vimeanzishwa na taasisi za kidini na vingine na taasisi za watu binafsi ambazo siyo za kidini hivyo kuwepo na tofauti ya changamoto kwa watoto hawa katika maeneo haya kutokana pia na utofauti wa aina ya malezi ambayo wamekuwa wakiyapata.

Mheshimiwa Spika, maisha hayana huruma na historia ya mwanadamu; Je, ni nini ubora na ufanisi wa utendaji wa maofisa wa Idara za Ustawi wa Jamii katika kuhakikisha kwamba, watoto wanaolelewa katika vituo hivi wanaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali hasa changamoto ya afya ya akili pamoja na kisaikolojia ili walau wanapotoka katika vituo hivi na kuwa vijana na watu wazima, waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha yetu ya kila siku. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Mayenga kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba mazingira ya maeneo wanayolelewa watoto yanatofautiana kutokana na kwamba yako mijini, vijijini, kwamba ni ya dini au binafsi na kwa maana hiyo kutokana na nilivyomuelewa mimi anaona kwamba, kuna utofauti kati ya malezi anayopewa mtoto katika sehemu hii na nyingine na hivyo kunaleta tofauti ya mtoto aidha pengine huduma inakuwa mbovu au pengine wengine wanapata huduma nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, kufuatana na ile sheria ambayo inaruhusu makao ya mtoto yaweze kuwekwa, Afisa Ustawi anaenda pale kukagua na kuna vigezo ambavyo vinatakiwa kuwekwa ili makao haya ya watoto yaweze kuwa, hivyo.

Afisa Ustawi anakwenda kuona sasa tofauti ya kwamba, mtoto pale anaona huduma pengine inatofautiana kati ya kijiji na mjini, mimi nadhani inategemea na uwezo wa pale au na huduma zinazotolewa.

Lakini cha msingi ni kwamba iwe makao yako mjini, vijiji au yawe ni ya dini au ya watu binafsi, Sheria inayomruhusu ni ileile moja na kwamba usimamizi wake ni ulele kufuatana na Sheria ya Mtoto ambayo imetoka kwa hiyo napenda tu nimueleze Mheshimiwa kuwa ustawi wa mtoto katika akili na kadhalika utategemea na yale mambo anayopata lakini pia kwa kuzingatia Sheria inasema nini kuhusiana na kutoa huduma kwa watoto hao katika makambi.

**MHE. DR.WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, suala la kulea watoto ni suala la uhai wa watoto hawa na tumepitisha katika Bunge hili Sheria ya kuwalinda watoto, jibu la Waziri halioneshi kwamba kuna umakini katika usimamizi wala ukaguzi; nina taarifa ya vituo ambavyo havijasajiliwa, nina taarifa ya vituo ambavyo vimeanzishwa na watu kwa jinsi walivyotaka, fedha za Wahisani zimeibiwa nina mfano halisi hata kwenye jimbo langu kama Kijiji cha Chemichemi nina mfano huo, Waziri anasema inakaguliwa;

Je, Waziri anaweza kulilettea Bunge hili ni lini mara ya mwisho ukaguzi kwa nchi nzima ulifanyika kuonesha kwamba, hawa watoto wetu wanahifadhiwa, wanalindwa, hadhi yao inalindwa na hata wale amba wanatumia nafasi hizi kuchukuliwa hatua? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Willbrod Slaa kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi Ustawi wa Jamii chini Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, maafisa wanatakiwa wakaguliwe kulingana na sheria ilivyo lakini huwa kuna utaratibu wa kupitia vituo na kuvikagua na vile ambavyo vinakidhi haja vinaendelea ambavyo havikidhi vinasimamishwa, sasa hivi tunavyo vituo vya kulelea watoto 85 na kuna vingine vimesimamishwa na ninaweza nikatoa mifano lakini ninachosema tu ni kwamba katika mambo yanayoendelea pale si rahisi kwa mfano; kukisimamia kituo kuona kwamba hata pesa wanazopata kutoka kwa wafadhili iwe ni kazi ya Ustawi wa Jamii kuona kwamba, pesa ile imeliwa namna gani, imetumika namna gani mimi ninachotaka kusema ni kwamba, kama wanapata ufadhili wao wanapata ufadhili kwa wafadhili wao walionao.

Kwa hiyo, sisi kama Wizara hatuwezi tukaenda tukaangalia pesa moja moja imetumika namna gani, nitakachowea kusema tu ni kwamba sisi kama Wizara, wajibu wetu ni kukagua vituo hivi na kuweza kuhakikisha kwamba, vinawekwa katika hali ambayo inastahili na kusema kwamba, lini mara ya mwisho nimeleta taarifa ya ukaguzi wa vituo hapa, siwezi nikatoa jibu kuwa mara ya mwisho vituo hivyo vimekaguliwa lini lakini pia tunaweza tukatoa hiyo ripoti ni livi vituo vimekaguliwa na lini havikukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini nakubali kwamba, kuna wakati mwingine utendaji unachelewa kidogo kwamba, hawaendi kukagua kwa hiyo mambo mengine unakuta kwamba, kuna utendaji mbovu au kuna wengine hawakidhi hilo nakubali lakini ninachosema, kusema sasa hivi kwamba, ni wangapi, mwisho lini, fedha kiasi gani itakuwa siyo rahisi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. kwa kuwa viko vituo vilivyoanzishwa na wageni kisha wageni hao wakavitelekeza na kurudi kwao kikiwemo kituo cha Kititimo kilichopo Singida Mjini ambacho sasa kinapata tabu ya kujiendesha kwa sababu hakina mtu wa kukihudumia;

Je, Serikali ina mpango gani na kituo hiki ambacho hakina mwelekeo na bado kina watoto yatima wengi? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba nimepokea taarifa kuhusu kituo cha Kititimo kwa sababu kama kimeachwa na mfadhili ameondoka sitakuwa na jibu la hapa, niseme tu kwamba tutalifanyiakazi halafu tuweze kuona tutawasaidia namna gani, ahsante. (Makofi)

Na. 33

### **Upungufu wa Watumishi Sekta ya Afya Nchini**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya afya nchini:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za dhati kuondoa upungufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Paschal C. Degera Mbunge wa Kondo Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sekta ya afya nchini inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi. Taarifa za tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa sekta ya afya nchini inapungukiwa na watumishi kwa wastani wa asilimia 62 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi wa sekta ya afya nchini kuanzia mwaka 2007 Serikali ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Madhumuni ya Mpango huu ni kusogea huduma za afya ya msingi karibu na wananchi.

Mpango huu una mikakati mingi, mkakati mmojawapo ni kuongeza idadi ya watumishi wa sekta ya afya ili kukidhi mahitaji. Katika utekelezaji wa mkakati huo, Serikali imeshughulikia na kutekeleza yafuatayo:-

- ¶ Kupanua vyuo vya kufundishia kwa kuongeza majengo, madarasa na hosteli pamoja na kuimariswa maktaba, maabara na vifaa vya kufundishia na kujifundishia.

Kutokana na mkakati huu, idadi ya wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo mbalimbali vya afya nchini vinavyozalisha watalaamu wa ngazi za kati kutoka 1,320 mwaka 2007 hadi kufikia 4,147 mwaka 2009/2010, lengo ni kudahili wanafunzi 6,500 kwa mwaka.

- ¶ Kuanzisha mpango wa mafunzo ya kuijendeleza kwa njia ya masafa (Distance Learning) ili kuwawezesha watumishi kuijendeleza wakiwa kwenye vituo vyao vya kazi.

- ⦿ Kuhamasisha sekta binafsi hususani mashirika ya dini kuanzisha vyuo vya watalaaam wa afya katika hospitali zao au kupanua vile vilivyopo ili viweze kuongeza udahili kwa maelewano kwamba kiasi kwa gharama kitabebwa na Serikali.
- ⦿ Kupunguza muda wa mafunzo ya afya kwa ngazi ya stashahada kutoka miaka minne hadi miaka mitatu na ngazi ya cheti kutoka miaka mitatu hadi miwili bila kuathiri kiwango cha taaluma.
- ⦿ Kurejesha mafunzo ya tabibu wasaidizi na wauguzi wasaidizi ngazi ya cheti ambayo awali yalikuwa yamefutwa.
- ⦿ Kulegeza masharti ya ajira kwa watalaaam wa kada za afya. Kundi hili hivi sasa linaajiriwa bila kufanyiwa usaili. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepewa jukumu la kuwapangia vituo vya kazi watumishi wa afya kwenye sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya.
- ⦿ Kuongeza mishahara ya watumishi wa kada za afya ili kuwavutia watalaaam wengi kuingia katika utumishi wa umma.

Kuongeza idadi ya vyuo vikuu vinavyotoa watalaaam wa afya kutoka vyuo vitatu mwaka 2005 hadi kufikia vyuo sita mwaka 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kuwa utekelezaji thabiti wa mikakati niliyoitaja hapo juu utatuwezesha kukabiliana na tatizo upungufu wa watumishi wa afya lililopo.

;;;;;;;;;;;;;;;;;;;  
;

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa katika kujibu swal la msingi amekiri kwamba jukumu la kuwapanga watumishi hadi Wilayani ni la Wizara yenyewe; na kwa kuwa Wilaya ya Kondoia ina matatizo makubwa sana ambayo yamesababisha baadhi ya zahanati zake kufungwa; je, Serikali haioni haja ya kuweza kuongeza watumishi wa afya katika Wilaya hii ili zahanati zilizofungwa ziweze kutoa huduma?

(ii) Pamoja na mikakati minge ambayo Wizara imeifanya ama inaitekeleza; ni lini Wizara ama Serikali inalenga kuondoa tatizo la upungufu wa Watumishi wa Afya Nchini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, jukumu la kupanga watumishi katika Wilaya nafikiri ni jukumu ambalo tunatakiwa tushirikiane na TAMISEMI. Sisi kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, jukumu letu tunapopata maombi kutoka Utumishi huwa tunawachukua watu waliokuwa katika soko kuwapeleka kule katika Wilaya na Wilaya ndio wanaopanga yupi aende wapi. Tatizo ambalo tunaliona sisi kama Wizara ni kwamba, tunapokuwa tumepata maombi mara nyingi tunapata watu tunawapeleka kwenye Halmashauri, lakini wakifika kule hawaripoti. Tatizo lingine unakuta katika soko hatupati maombi ya watu ambao wanataka kupata hizi ajira.

Nataka kusema kwamba, sisi kama Wizara huwa tunachukua watu waliohitimu kutoka vyuo na kuwapangia kazi na wale ambao huwa wanakuja kwenye soko tunawapangia maeneo ya kwenda kufanya kazi kutokana na maombi yaliyotoka Utumishi.

Ninachotaka kusema kwa kuchanganya na suala lake la pili ni kwamba, kama nilivyosema katika jibu langu la swal la msingi; Serikali ina mikakati hiyo na tumefanya jitihada ya kuweza kuona kwamba udahili wa watoto tunataku uifikie 6,500 kila mwaka. Kwa hiyo, tunachokifanya hapa ni kuhakikisha kwamba, tunawashauri watoto wanaofaulu masomo ya sayansi waombe kuingia katika vyuo vyetu hivi vya afya ili hatimaye tuweze kupata udahili huu wa 6,500 na hatimaye wahitimu watakuwa wengi kiasi kwamba wataweza kwenda katika yale maeneo ya kutolea na huu upungufu hautajitokeza. Ni matumaini yetu kwamba, mpango huo wa miaka 10 utakapomalizika, bila shaka tutafanikiwa kiasi kikubwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda hauturuhusu, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kabla hatujafika huko, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge ambao ni wateja wa dawa za asili ambazo zilisitishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Saba baada ya purukushani pale zimerejeshwa tena. Kwa hiyo, wale wanaopenda dawa za asili basi huduma inaendelea kama kawaida. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 34

#### **Rushwa na Upendeleo Katika Jeshi la Wananchi**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lina utaratibu wa kutoa ajira ya Wanajeshi lakini wanaopewa dhamana ya kuandikisha vijana hao hasa kwa upande wa Tanzania Zanzibar wamegubikwa na rushwa na upendeleo wa upande mmoja; kwa mfano, vijana wapatao 20 walifaulu katika hatua zote za usaili na kusafirishwa hadi Dodoma kwenye mafunzo ya Kijeshi lakini ghafla walirudishwa Tanzania Zanzibar na vyeti vyao halisi vikazuiliwa Kambini jambo ambalo limezua wasiwasi kuwa pengine vyeti hivyo wamepewa vijana wengine:-

(a) Je, Serikali haioni kwa hali hii ya rushwa na upendeleo inawanyima haki vijana wenye uwezo?

(b) Je, kwa nini vijana hao waliorejeshwa kutoka Dodoma hawakurejeshewa vyeti vyao na ni nini hatma ya vyeti hivyo?

(c) Je, ni sababu gani ya msingi iliyofanya vijana hao wote 20 kuondolewa Kambini na badala yake wakaingizwa wengine?

#### **NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatoa upendeleo katika uandikishaji wa vijana wa kuijunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania. Uandikishaji wa vijana wapya Jeshini hufanywa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa ambazo hutoa fursa sawa kwa wote. Wale wasio na sifa zinazotakiwa hawapokelewi.

(b) Mheshimiwa Spika, vijana anaowataja Mheshimiwa Mbunge, walibainika kuwa na vyeti vyenye dosari na vikapelekwa Baraza la Mitihani kwa uhakiki. Kwa mujibu wa utaratibu wa Baraza la Mitihani, vyeti vyaa kughushi vinapobainika hubakizwa Baraza la Mitihani kwa kuwa huweza kutumika kama ushahidi Mahakamani pindi wahusika wanaposhtakiwa

(c) Mheshimiwa Spika, sababu za vijana hao kuondolewa kambini ni kutokana na kughushi vyeti na baadhi yao kuwa na matatizo ya kiafya. Ni vyema Mheshimiwa Mbunge akaelewa kwamba, kutumikia Jeshi la Ulinzi la Wananchi huhitaji sifa maalum za kielimu na afya njema ili kuweza kutekeleza majukumu ya kijeshi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, tabia ya kughushi vyeti iliyobainika kwa vijana hao ni kielelezo cha ukosefu wa uaminifu na uadilifu na hivyo basi kukosa sifa muhimu za msingi zinazohitajika katika utumishi ndani ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

ambalo kama Mheshimiwa Mbunge anavyofahamu, linahitaji askari waadilifu na wenyetabia njema.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sisemi kwamba nimeridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kama alivyosema, siyo kweli na mimi nasema siyo kweli kwamba, vijana hao wamegushi vyeti na ndani ya vijana hao 20, vijana wanenye wanatoka katika Jimbo langu la Dimani katika Tawi la CCM Fumba. Nimesema si kweli kwa sababu nakala za vyeti hivyo nimeshampa Mheshimiwa Waziri ili avifanyie kazi. Vijana hao walikuwa katika Kambi ya Mafunzo miezi miwili na kabla ya hapo vijana hao huwa wanapitishwa katika sekta zote za kiafya na mambo mengine.

(i) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba analidanganya Bunge na analidanganya Jimbo langu kwamba vijana wangu walighushi vyeti wakati vyeti hivyo ni halali?

(ii) Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatana nami katika hizo Taasisi ambazo amezisema ili kuona kama vijana hawa hawakutendewa haki kwa kunyimwa nafasi yao ambayo tayari wamekwishapewa ya miezi miwili kuwekwa Kambini halafu ikatolewa; narudia kwamba Mheshimiwa Waziri afuatane na mimi katika sekta zote tuhakikishe vijana hawa wanapata haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, naomba kwa mara nyingine kukuthibitishia na kulithibitishia Bunge hili kwamba, niliyosema yote ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale wote ambao tulipeleka vyeti vyao Baraza la Mitihani, Baraza la Mitihani ndio lenye wajibu wa kutambua cheti kilichoghushishi na kisichoghushishi na ndilo lililotambua vyeti hivyo. Siyo tu niko tayari kwenda na Mheshimiwa Hafidh Ali kwenye Taasisi hiyo ya Baraza la Mitihani, lakini pia awe tayari kuona mchakato wa kuwapeleka Mahakamani ukitekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kwa suala la kiafya vile vile naomba kulithibitishia tena Bunge lako kwamba, waliogundulika kuwa na matatizo ya kiafya walikuwa watano, wanenye kati yao ni wanawake ambao wote walibainika kuwa ni wajawazito na mmoja aligundulika kuwa na matatizo ya kawaida. Katika hao wanawake; wawili walitoka Zanzibar na wawili walitoka Tanzania Bara. Ni wajibu wa Wizara ya Ulinzi kujali afya ya mama na mtoto. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Na. 35

#### **Uanzishwaji wa “Sites” za Utalii Kusini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kukuza utalii wa ndani na nje katika Mikoa ya Kusini na ili kutumia vizuri vivutio vilivyopo kwenye fukwe za Bahari, Mambo ya Kale na Mapango:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa katika Mbuga ya Pori la Msanjesi - Masasi ili kuunganisha utalii wa fukwe na kutembelea wanyama na hivyo kushawishi watalii wengi kutembelea Mikoa ya Kusini?

(b) Je, kwa nini Shirika la Hifadhi la Wanyamapori (TANAPA) halianzishi hifadhi katika eneo hilo ili kuongeza nguvu katika uanzishaji na uimarishaji wa hifadhi ya kwanza katika maeneo ya Kusini?

#### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kabla ya kuanzisha Hifadhi ya Taifa, vigezo na utaratibu ufuatao huzingatiwa:-

- Jamii na uongozi wa eneo husika wawe tayari kukubali eneo hilo kuwa Hifadhi ya Taifa kwa kuanzisha mchakato kuanzia ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa na kuwasilisha mapendekezo Wizarani kwa hatua zaidi.

- Kusiwe na uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye eneo husika pamoja na maeneo yanayozunguka.

- Eneo husika linatakiwa liwe na ukubwa wa kutosha ambao utawezesha mifumo ya kiikolojia kufanya kazi bila vikwazo. Kwa mfano, kama kwenye eneo husika kuna wanyama wakubwa kama tembo, wanyama hao wanatakiwa wapate sehemu za kuzalia pamoja na kupata maji na malisho pasipo na matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ipo tayari kuanza mchakato wa kupandisha Pori la Akiba Msanjeshi Masasi kwa kuwa linakidhi vigezo muhimu kwa ajili hiyo. Hata hivyo, Wizara haijachukua hatua hiyo ili kutoa nafasi kwa wananchi wenyewe kuanzisha mchakato na kuridhia kuititia vikao vyao vya Wilaya na Mkoa.

Shirika la Hifadhi la Taifa litawajibika baada ya utaratibu wa kisheria wa uanzishwaji Hifadhi ya Taifa kukamilika na wao kukabidhiwa Hifadhi hiyo kwa kuwa wao ni wasimamizi tu.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa kujibu vizuri suala hili. Pamoja na hayo kuna maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa suala hili liliwahi kufikishwa katika Kikao cha Ushauri cha Mkoa (RCC) Mtwara; na kwa kuwa kama alivyosema kwamba Pori hili linakidhi vigezo vingi vinavyoweza kuiwezesha liwe Hifadhi ya Taifa; je, Wizara yake ina mipango gani kuusaadia Mkoa wa Mtwara ili hifadhi hii au pori hili liweze kuwa hifadhi mapema iwezekanavyo? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa Mkoa wa Mtwara na hasa Mtwara yenye hivi sasa inakua kwa kasi sana kutokana na rasilimali nyingi zilizogunduliwa hivi karibuni kwa mfano gesi, mafuta na kadhalika na kuwafanya wageni wengi wafike katika Mkoa wa Mtwara; je, Wizara yake inatambua hali hii na inafanya nini ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na Kitengo cha Utalii cha TTB au Wizara yenye ili kuibua mipango mbalimbali itakayokidhi matakwa ya watalii wengi wanaokuja katika Mkoa wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mrope, kwa kutusaidia sana katika jambo hili kwa sababu mbali na kuuliza swali lakini kwa hakika amekuwa akiliuliza mara kwa mara na naamini haya ndiyo matakwa ya Wananchi wa Mkoa wa Mtwara. Kwa kuwa tayari wameshalijadili na wamelifikisha kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Wizara yangu sasa iko kwenye hatua ya kulipokea kutoka ngazi hiyo.

Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mkoa sasa ulilete Wizarani kwetu ili sisi tuweze kufanya hatua za kitaalamu zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kusaidia kwa ujumla kuimarisha utalii wa Mkoa wa Mtwara hasa kwa kuzingatia wageni wengi wanaotembelea eneo hilo, tayari Wizara ilishafanya utafiti wa kubainisha vivutio vyta utalii vilivyoko Mkoa wa Mtwara na Kanda nzima ya Kusini mwaka 2001. Vigezo na maeneo mengi ya vivutio yalishabainishwa na tayari sasa hivi tumeshaanza kuhamasisha wawekezaji ili wawewe kuwekeza na hatimaye kushirikiana na utalii wa eneo hilo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wengine wa eneo hilo kwa sababu sasa hivi mawasiliano yameimarika basi waungane mkono na Wizara kuanza uwekezaji na sisi tuko tayari kuendelea kutangaza vivutio vyao.

Na. 36

**Uendelezaji wa Visiwa vya Gozi, Kerebe, Bumbile,  
Kome na Nyabulo kwa Utalii**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE aliuliza:-**

Kwa kuwa Serikali ina mikakati mizuri ya kuboresha maeneo mbalimbali ya kiutalii ikiwa ni pamoja na Visiwa vya Gozi, Kerebe, Bumbile, Kome na Nyabulo:-

Je, Serikali itaboresha lini Visiwa hivyo ili viwe sehemu ya utalii kwa lengo la kuchangia kwenye Pato la Taifa?

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii iliandaa mpango wa utambuzi na uendelezaji wa vivutio vya utalii vilivyoko Kagera mnamo mwaka 2001. Wizara iliandaa mpango huo baada ya Wataalamu wa Wizara kutembelea Kagera na kubainisha vivutio vingi vikiwemo visiwa alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

Katika visiwa hivyo ni kisiwa cha Bumbile pekee kilichoonekana kuwa na *Tourism Potential* kubwa ukilinganisha na visiwa vingine. Tayari Wizara imeshaandaa taarifa na vijitabu viwili viitwavyo *Tourism Potential of Kagera* na kingine cha *Tourism Attractions of Kagera Region*, vinavyoainisha vivutio kwa kila Wilaya. Vijitabu vyote hivi vinaelezea pamoja na mambo mengine, vivutio vingi kikiwemo Kisiwa cha Bumbile. Vijitabu hivi sasa vinasambazwa kwa wadau kwenye maonesho ya utalii ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu tayari imehamasisha Wananchi wa Kagera ambao wameunda chama cha kuendeleza utalii kiitwacho *Kagera Tourism Development Association*, ambacho kimekuwa kikifanya kazi nzuri sana na kutangaza vivutio vya utalii kwa kushirikiana na Wizara yangu kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Tayari chama hiki kwa kutumia taarifa ya utafiti iliyandoaliwa na Wizara yangu, imeandaa Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa kulinda na kuendeleza vivutio vya utalii vilivyoko Kagera. Mpango Mkakati huu umekuwa ukitekelezwa na chama kwa kushirikiana na wadau wengine kwa kipindi chote hicho. Kwa upande wa ulinzi wa rasilimali zilizoko kwenye visiwa hivyo, wananchi wamekuwa wakihamasishwa kutunza maeneo hayo na kupitia Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi, visiwa vilivyo vingi tayari sasa hivi ni *Beach Management Units* na kwa sababu ni kambi za wavuvi, hali ya afya imeboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu tayari imeshachukua hatua za kuendeleza utalii Kanda ya Ziwa, ambapo mwaka 2006, Siku ya Utalii Duniani iliadhishwa Bukoba kwa lengo la kuutangaza Mkoa huo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kama *Kiloyera Tours and Consulting* ambao ofisi zao ziko Bukoba na Shirika la Maendeleo la Uhlanzi SNV, wameanza kuandaa Makongamano (*Tourism Forums*), kwa kila Mkoa wa Kanda ya Ziwa. Mwezi Novemba, 2009 kulikuwa na *Tourism Forum* ya Mkoa wa Mwanza.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa majibu yanakuwa mazuri kuliko vitendo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa katika Kisiwa cha Bumbile kuna sehemu moja ina maghofu waliiyokuwa wanakaa Wajerumani ambayo yakiboreshwaa na Serikali tutapata kipato

kizuri katika Mkoa wetu wa Kagera pamoja na kuboresha usafiri; naomba Waziri atujibu atatusaidiaje kuyaweka vizuri maghofu ili tupate utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuonesha kwamba, eneo hili ni muhimu na kama nilivyosema hata sisi tumeshalitambua. Hatua ambazo tumekwishakuzianza sasa hivi ni kuwashamasisha wawekezaji na kwa kiasi kikubwa, Wizara inaratibu shughuli hizi. Uwekezaji unafanyika na sekta binafsi kwenye hoteli na hata kwenye vyombo vyaa usafiri. *Tour operators* ni sekta binafsi, kwa hiyo, tunachokifanya ni kuwashamasisha na tayari kuna watu wameshaanza kuonesha nia ya kuwekeza katika usafiri na kuanzisha aina fulani ya utalii kwenye kisiwa hicho. Mazungumzo yako kwenye hatua nzuri, naomba Mheshimiwa Mbunge atuamini na atupe nafasi tuweze kukamilisha tuliyoyaanza.

Na. 37

### **Ugonjwa wa Minazi Katika Wilaya ya Kilwa**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa minazi ni tatizo katika Wilaya ya Kilwa maeneo ya Singino, Mteja, Mingumbi na Kiwawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulinusuru zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kunyong'onyea kwa minazi (*Coconut Letho Disease*), umekuwa ni tatizo katika Wilaya ya Kilwa kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge na limekuwa ni tatizo la muda mrefu tangu miaka ya 1960. Kwa sasa ugonjwa huu umeathiri pia maeneo ya Wilaya za Rufiji na Mkuranga. Utafiti kuhusu ugonjwa huu umebaini kwamba, vijidudu aina ya *pytoplasma* vinavyosababisha ugonjwa huu havitibiki kwa kutumia madawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo ili kulinusuru zao hilo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ina mipango ifuatayo:-

(a) Kuzalisha miche ya minazi ya asili ambayo hustahimili ugonjwa huu. Mpango huu unaendelea kutekelezwa katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Chambezi, Wilayani Bagamoyo.

(b) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau wa zao la minazi kuhusu namna ya kutambua minazi ilioathirika na ugonjwa huu na kuwashauri kuikata na kuichoma moto mara moja.

(c) Kuhamasisha wakulima kuhusu kupanda mbegu au miche itokanayo na minazi iliyothibitika kuwa na ustahamilivu wa ugonjwa huu.

(d) Kuzishauri Halmashauri za Wilaya zinazolima minazi kuvivezesha vikundi vyta wakulima vyta kuanzisha vitalu vyta miche bora ya minazi ili kurahisisha upatikanaji wa miche ya minazi kwa wakulima wengine katika maeneo yao.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa ugonjwa huu inasemekana uko nchini toka 1960; je, Waziri anasemaje kwa kuwa mwaka 1960 mpaka leo takriban miaka 45 na amesema kwamba kuna kituo kimoja cha utafiti ambacho kiko Chambezi Wilayani Bagamoyo; je, Serikali inasemaje kuhusu kuongeza vituo vyta utafiti maeneo ya Kilwa ili tuweze kuinusuru minazi yetu?

(ii) Wizara ina mpango gani wa kutokomeza miche mibaya ambayo haistahimili magonjwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu ultambulika duniani mwaka 1905 na pia uliingia Tanzania mwaka 1905, lakini kuanza kusambaa na kuleta madhara makubwa ni mwaka 1960. Ugonjwa huu kwa sasa unaweza kutumia minazi ile ya *East African Tall* ila inaweza kustahimili kwa asillimia 30. Nchi kama Jamaica walijaribu lakini baada ya miaka 15 minazi yao ilikufa, kuonesha kwamba vijidudu hivi vinabadilika kutokana na mazingira na vinatofautiana kutokana na nchi moja hadi nyingine.

Sasa hivi Kenya, Mozambique na Ghana bado wana tatizo hili kubwa lakini maeneo ya India na Philipines wao wana ugonjwa mwingine ambapo vituo vyetu vilileta minazi kutoka maeneo hayo kwamba, labda minazi hiyo itafaa Tanzania lakini minazi ile ilikufa haikuweza kustahimili ugonjwa huu hapa Tanzania.

Kwa hiyo, katika suala la kuongeza kituo kule Kilwa, nadhani kinachotakiwa hapo ni kuongeza uwezo wa kituo kilichoko Chambezi ili kiweze kuzalisha miche zaidi na ili utafiti uweze kuendelea vizuri zaidi basi huko mbele tutaangalia kama tunawenza kuongeza maeneo gani mengine.

Mheshimiwa Spika, minazi inayofaa kwa sasa hivi ni minazi ya *East African Tall*, kwa hiyo, tunazishauri Halmashauri ziweze kuanzisha vitalu vyta minazi hii ili viweze kuwasaidia wakulima wa minazi na minazi ile chotara iliyokuwa imeanzishwa mwanzoni imeonesha kwamba haifai kabisa.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi nina swali moja dogo la kuuliza. Kwa kuwa utafiti umeshaonesha kwamba hakuna uwezekano wa kuuondoa ugonjwa huu wa minazi; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kwamba kuna minazi mingine ambayo inaweza kupandwa na kutoa ile ya zamani ambayo ina maradhi hayo na Halmashauri ziweze kusaidia; je, ni lini harakati hizi zitaanza kwa kuwa wananchi wa Kilwa na Mkoa wa Kusini, Mikindani Lindi nzima, wanategemea zao hili kama zao la biashara; itaanza lini *process* ya kuleta hii minazi na kuisambaza katika maeneo yetu na kung'oa ile ya zamani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, niseme katika utafiti wowote hatuwezi kusema kwamba imeshindikana. Tunasema kwamba, bado tunaendelea na utafiti hatimaye tuweze kugundua dawa inayoweza kutibu ugonjwa huu. Nadhani tunakumbuka kwamba, hata Ugonjwa wa UKIMWI uliingia mwaka 1980, lakini mpaka sasa hivi hatujapata dawa wala chanjo. Kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba imeshindikana, bado tunajitahidi tuweze kupata dawa ama chanjo ya magonjwa kama hayo.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuchukua miche kutoka kwenye kituo chetu linaendelea, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri yake waweze kutenga fedha kutoka DADPs waweze kuchukua mbegu za minazi ili waweze kuongeza vitalu katika Halmashauri zao.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda unatutupa mkono. Swalii la mwisho ni la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

Na. 38

**Viwanda vya Kahawa Vinavyoweza  
Kuwasaki Wakulima**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Viwanda vya Kahawa kama vile *Mbozi Coffee Curing Company* na *Moshi Coffee Curing* vilijengwa na Serikali kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika kama vile Mbozi MBOCU, Isayula, MBICU, KNCU na kadhalika; na kwa kuwa baadhi ya vyama hivyo kwa sasa havifanyi kazi zake kwa ufanisi kabisa kama vile MBOCU:-

(a) Je, wakulima wa Zao la Kahawa Wilayani Mbozi wanafaidikaje na kuwepo kwa Kiwanda hicho Wilayani kwao?

(b) Je, ni nani mwenye wajibu wa kusimamia na kukarabati Kiwanda hicho ambacho kwa sasa mitambo yake imechakaa sana pamoja na nyumba za watumishi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Kiwanda cha Kahawa cha Mbozi uligharamiwa na Serikali kwa msaada wa Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya, pamoja na michango ya Vyama vya Ushirika kwa njia ya makato ya fedha za mauzo ya kahawa ya wakulima. Michango ya Vyama vya Ushirika ilithamanishwa kuwa hisa zao katika Kiwanda.

Madhumuni ya ujenzi wa kiwanda hicho yalikuwa ni kupunguza gharama za kusafirisha kahawa ghafi kwa umbali mrefu kwenda kukoboa katika Kiwanda cha Kahawa cha Moshi. Hivyo, kuwepo kwa kiwanda hicho kulilenga kumnufaisha Mkulima wa Kahawa wa Wilaya ya Mbozi kwa kumpunguzia gharama na kumwongezea kipato.

Aidha, kuwepo kwa kiwanda hicho kulilenga kuwapa motisha wakulima wa kahawa Wilayani Mbozi, kuongeza uzalishaji wa kahawa pamoja na kutoa ajira kwa wakulima wa Wilaya ya Mbozi na wengineo. Malengo haya bado ni muhimu.

(b) Mheshimiwa Spika, wajibu wa kusimamia na kukarabati Kiwanda cha Mbozi ni Bodi ya Wakurugenzi wa Kiwanda hicho kwa kutumia mapato yatokanayo na ushuru wa kukoboa kahawa. Pakiwe po na mpango mzuri wa biashara , Bodi inaweza kuomba mkopo kutoka vyombo vya fedha ili kukarabati mitambo na majengo yaliyochakaa. Serikali itaendelea kuhimiza Bodi ya Kiwanda iandae mipango ya biashara mizuri ili ikopeshwe na kukarabati kiwanda hicho cha Mbozi. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwahamasisha wakulima wa kilimo cha kahawa Wilaya ya Mbozi waongeze uzalishaji na kukitumia kiwanda chao kama ilivyokuwa imekusudiwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, naomba niseme kwamba sijaridhika sana na majibu ya Serikali kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake anasema kwamba, michango ya wananchi pamoja na Serikali na Vyama vya Ushirika na Wafadhili ndiyo iliyowezesha kujenga kiwanda kile lakini leo kile kiwanda ni kama kimetelekezwa; wakati kinaanza kilikuwa kina wafanyakazi wa kudumu zaidi ya 200 lakini leo kina wafanyakazi wa kudumu chini ya 20! Hata hivyo, gharama za ukoboaji kahawa kiwandani pale hazina tofauti na viwanda vingine, kwa mfano, Chalima na City Coffee pale Mbeya:-

(i) Je, ni faida gani sasa ambazo mwananchi huyu wa Mbozi aliyechangia kujenga kiwanda hiki pamoja na Viwanda vya Ushirika vinapata kwa sababu ni kama sasa hakina maana?

(ii) Naomba Serikali iseme leo bayana ni nani hasa mmiliki wa kiwanda kile kwa sababu hata hawa Mawaziri ambao anasema walisaidia kujenga na michango yao

ikageuzwa kuwa hisa leo haieleweki wanaripoti kwa nani na tukipata matatizo tumpate nani kwa sababu ukienda kwa Bodi hawaelezi chochote kuhusu umiliki wa kiwanda hiki kwa Serikali? Naomba Serikali itupatie majibu mazuri ili tuweze kuridhika.

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri kujibu; umeme unaoingia humu Ukumbini kila mnapoona mabadiliko maana yake umeme wa TANESCO umekatika na inabidi muwe na muda kidogo wa umeme wa *standby generator* uweze kuwaka. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi nini kinatokea humu; mara giza kidogo mara mwanga ndiyo hali hiyo. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nitaanza na swali la pili kwamba, nani mmiliki wa kile kiwanda. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Zambi kwamba, mmiliki wa kiwanda hiki ni Vyama vya Ushirika katika eneo hilo wanaolima kahawa kwa asilimia 68. Serikali inamiliki asilimia 32 na kiwanda hiki kina Bodi ya watu saba; wawili kutoka Serikalini na watano kutoka kiwanda hiki.

Sasa kuhusu gharama za ukoboaji; gharama za ukoboaji wa kilo moja ya kahawa ni shilingi 60 na gharama hii ni sawa na viwanda vingine vya Mkoa wa Mbeya lakini ni chini ya Kiwanda cha Moshi ambacho kwa *organic coffee* wanakoboa kwa shilingi 100 kwa kilo na shilingi 60 hadi 72 kwa kilo kwa kahawa ya kawaida. Kwa hiyo hizi shilingi 60 zinatumika katika gharama za umeme, gharama za upakuaji na upakiaji pamoja na kushona mifuko ya kuwekea kahawa. Kwa hiyo, katika uendeshaji wa kiwanda hiki bado bei hii ni ndogo na niseme kwamba kiwanda hiki bado kinaendelea vizuri na kina uwezo wa kukoboa kahawa yote inayopatikana Mbeya na uzalishaji wa kahawa sasa hivi Mbeya ni mdogo kuliko uwezo wa kiwanda hiki.

Habari nzuri ni kwamba, tayari kiwanda hiki kimeagiza mitambo miwili kutoka Brazil inaingia Februari kwa ajili ya kuongeza uwezo zaidi na kitakuwa cha kisasa zaidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali sasa umepita. Kabla sijasoma matangazo, naomba kutoa ufanuzi ufuatao kuhusu nukuu za magazeti kuhusu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Juzi magazeti yalimnukuu akisema: “*Kelele za Walimu haziitishi CCM, madai ya Walimu hayaithi CCM na lingine likasema Hatutishiki.*” Sasa nimeagiza Hansard, maneno halisi aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kama ifuatavyo:-

Nanukuu Hansard: “*Mheshimiwa Spika, mchakato katika utumishi hauwezi kuisha na ndiyo maana tumeongea na Mheshimiwa Celina Kombani ameagiza kusitokee tena malimbikizo. Watalipwa tu, lakini hakuna tishio la Chama cha Walimu kukisulubu Chama cha Mapinduzi.*” Naibu Waziri anasema hakuna tishio; yaani taarifa alizonazo Wizarani halipo hilo tishio, magazeti ndiyo yananukuu kwamba CCM ndiyo inasema haitishiki. Sasa uandishi huu nawahisi wenzetu wanaotoa taarifa humu watende haki maana hii ilikuwa ni kuwachokoza tena walimu badala ya kuiweka hali halisi kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana. (*Makofî*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SAID A. ARFI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Arfi, Kanuni?

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7). Ninaomba mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 30(4)(m) kimeeleza bayana shughuli zitakazofanywa na Bunge kwa mpangilio ulioelekezwa katika kifungu kidogo cha nne. Lakini kifungu cha 37(7) kinatoa maelekezo kwamba, taarifa zitakazowasilishwa kwenye Bunge zitajadiliwa. Jana tumepata ratiba ya shughuli za Mkutano huu, Taarifa za Kamati zimepangwa zote tarehe 12 na tutapokea Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu RITES, TICS na pia Taarifa ya Richmond na kupokea Taarifa ya Madini na Nishati kuhusu Kiwira. Kwa busara yako na kwa mujibu wa Kanuni; je, unadhani kwamba Bunge litapata fursa za kuzijadili hoja za Kamati hizi?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sielewi wasiwaso wa Mheshimiwa Arfi ni upi kwa sababu shughuli zimepangwa, taarifa zitatolewa na kujadiliwa. Sikupenda nimzuwie kuendelea kutokana na kuathiri Kanuni inayozuia Mbunge kuwashisha shughuli ambazo bado ziko mbele yetu. Lakini nitaendelea kuwa makini na kuhakikisha kwamba, mnipata nafasi ya kutosha ya kujadili taarifa hizo.

Matangazo, wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia, ambao ni Ndugu Dashudi Mdeme, Mkurugenzi Msaidizi Wizarani, Ndugu Daudi Saveri, Katibu Sekretarieti ya Ajira na Ndugu Gideon Malabeja, Afisa Tawala Mkuu.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ambaye ni Ezekiel Clement. Tuna wageni wa Mheshimiwa John Samwel Malecela na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kutoka Majimboni mwao kama ifuatavyo: Wapo Wenyeviti wa Kata 14 wa CCM za Jimbo la Same Mashariki pamoja na Makatibu 14 wa Kata hizo. Wageni wetu kutoka Same ambao ni wageni wa Waheshimiwa hao wawili kwa sababu zilizodhahili kabisa, naomba wasimame tafadhali. Karibuni sana na kwa niaba ya Wabunge wenzangu, tunawapeni pole sana kwa maafa yaliyowapata kwa udongo kuperomoka katika masika ile ya mwaka jana.

Wageni hao hao sasa wa upande wa pili wa ubavu ni Wenyeviti 16 na Makatibu 16 kutoka Jimbo la Mtera. Ahsanteni sana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wawili wanashabihiana na pia wapigakura kutoka Majimbo haya mawili wapo karibu karibu. Tunawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na Mzee Malecela na Mama Anne Kilango. Ahsanteni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama ni wanafunzi 74 kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, wakiongozwa na viongozi watatu ambao ni Thomas Mwikuka, Dean of Students, Advocate Calvin Mandapi, ambaye ni Assistant Lecturer na Ndugu Nuhu Suleiman, Rais wa Serikali ya Wanachuo; wale pale. Naomba

msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Ahsante sana, karibu sana. Tunatambua kuwa tuna upungufu mkubwa wa Mahakimu, tunatazamia mtafanya kazi yenu vuziri ili muweze kutusaidia katika eneo hili la kusimamia haki. Karibuni sana na tunawatakia mema.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Luckson Mwanjale wa Mbeya Vijijini, ambao ni Mwl. Akimu Chaula, naomba asimame. Wageni wa Mheshimiwa Dunstan Mkapa ni Ndugu Merry Kapiligala kutoka Kisasa Dodoma na Ndugu Bahati Semunyo naye kutoka Kisasa Dodoma. Mheshimiwa Mkapa hakueleza uhusiano wake na wageni hawana wala hakusema wanatoka Jimboni lakini kanuni zinaruhusu tu Watanzania wote wanawenza kuja hapa. (*Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Diana Chilolo ni wanafunzi wa shahada ya kwanza kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, ambao ni Mussa Sima, Mhoja Kulwa, Scola Mtalo, Mwanahamasi Mwinjori na Godwina Mlyoto. Ahsante sana tunawatakia mafanikio mema katika masomo yenu ya Chuo Kikuu. Mgeni wa Mheshimiwa Zainabu Matitu Vullu ni Bi Sharifa Matitu kutoka Chuo cha Mahakama Lushoto; tunaomba asimame, ahsante sana.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi leo katika Ukumbi Namba 231 katika ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Mheshimiwa Omar Kwaang'w Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii saa saba mchana leo anaomba Wajumbe wa Kamati hii mkutano katika ukumbi namba 227.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane saa saba mchana kwenye Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani wanakutana na wadau; ni Mkutano muhimu kwa Muswada ulio mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kutoka magazeti ya The Economist and USA World Today, wamepitia taratibu zote za vibali kwa waandishi wageni na wapo kwenye maeneo haya ya Bunge wakifanya hojaji mbalimbali na kuongea na Waheshimiwa Wabunge kama viongozi wa nchi hii. Kwa hiyo, mkiona wageni hawa muelewe kwamba, wamefuata taratibu zote za kisheria na wanajaribu kutoa toleo maalum katika magazeti yao ili kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo ni halali kabisa tuwape ushirikiano wageni wetu hao waandishi wa habari.

Mwisho, saa saba na nusu leo katika Ukumbi wa Spika, kutakuwa na Mkutano wa Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Hili ni

tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Wabunge wa CCM. Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Katibu hatua inayofuata.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)*)  
No. 3 Bill, 2009)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye kuitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Bill, 2009*).

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa majaliwa na neema zote ndogo na kubwa alizonijalia. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kutoa hotuba mbele ya Bunge hili tangu nilipoteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu. Ninauchukua uteuzi huu kama nafasi yangu nyingine ya pekee ya kuwatumikia Watanzania kwa ufanisi, umakini na uaminifu kwa mujibu wa kiapo changu ambacho kamwe sitakisaliti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tangu Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge hili, yametokea matukio kadhaa: Taifa limempoteza mmoja wa waasisi wake, Mzee wetu, Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Mzee Rashid Mfaume Kawawa, ambaye alifariki dunia tarehe 31 Desemba, 2009. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Vita Kawawa na watoto wengine wa marehemu, jamaa na Watanzania wote kwa msiba huo na kuwaomba tumwombee huyo Mzee wetu kwa Mwenyezi Mungu ili ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Aidha, ninawaomba Viongozi wote na Watanzania wote, waige kwa kutenda na waishi maisha kama yale ya mzee wetu.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia kutumia fursa hii kutoa pole na rambirambi zangu kuitia kwa Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika hasa kwa Wananchi wa Iringa, Dodoma, Same, Kilosa, Kigoma na maeneo mengine ya nchi ambayo yamekumbwa na maporomoko na mafuriko yaliyosababisha vifo, majeruhi na upotevu wa mali na mazao. Kwa Wananchi wa Mikoa ya Arusha na Manyara ninatoa pole kwao kutohana na kiangazi kikubwa kilichosababisha vifo vya mifugo yao. Vile vile na Wananchi wa sehemu nyingine nchini, ambao bado hawajapata mvua za kutosha. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie neema tele, aepushe maafa na atujalie mvua za kiasi.

Mheshimwia Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Mara na hasa Viongozi wa Wazee wa Mila katika Tarafa ya Kiagata, hususan Kata ya Buswahili, kwa ukarimu wao kwangu na kwa kuniruhusu na kunikaribisha kuwa katika kundi lao la uongozi wa mila. Kama nilivyowaambia, ninaamini kwamba mila na desturi nzuri zinapaswa kudumishwa na kutekelezwa sawa na sheria za nchi kwa ajili ya maendeleo ya jamii zetu. Hata hivyo, kama kutakuwa na migongano, basi sheria za nchi ndizo zitakazozingatiwa. Ninaomba tulizingatie hili; vinginevyo, tutakuwa tunavunja sheria na tukivunja sheria tutashughulikiwa kisheria, atakayewashughulikia ni mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaeleza maudhui ya Muswada huu, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wote wa ofisi yangu na hususan Naibu Mwanasheria Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya kuniwezesha kufanya kazi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa haraka, kwa viwango na utulivu. (*Makofi*)

Ninamshukuru kwa aina ya pekee, Mwandishi Mkuu wa Sheria na Maafisa Waandishi wa Sheria, kwa kutuwezesha kuwa na kazi za Bunge za kutosha. Aidha, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpawawa na kupitia kwake, kwa Waheshimiwa Wabunge walio Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa ushirikiano na ushauri wao mzuri waliotupa wakati wote wa kuupitia na kuujadili Muswada huu. Nawashukuru sana; maoni na Ushauri wao kwa kiasi kikubwa vimesaidia kuuboresha Muswada huu na kufanya marekebisho yaliyoambatishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unatoa mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho Sheria kumi na tatu zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai, Sura ya 20 (*The Criminal Procedure Act, Cap. 20*);
- (ii) Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara, Sura ya 315 (*The College of Business Education Act, Cap. 315*);
- (iii) Sheria ya Kudhibiti Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 (*The Economic and Organized Crime Control Act, Cap. 200*);
- (iv) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 (*The Employment and Labour Relations Act, Cap. 366*);
- (v) Sheria ya Kurejesha Watuhumiwa Waliofanya Makosa Nje ya Nchi, Sura ya 368 (*The Extradition Act, Cap. 368*);
- (vi) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (*The Land Act, Cap. 113*);
- (vii) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (*The Land Disputes Courts Act, Cap. 216*);
- (viii) Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura ya 395 (*The National Health Insurance Fund Act, Cap. 395*);
- (ix) Sheria ya Hati za Kusafiria, Sura ya 42, (*The Tanzania Passports and Travel Documents Act, Cap. 42*);

- (x) Sheria ya Mbegu, Sura ya 308 (*The Seeds Act, Cap. 308*);
- (xi) Sheria ya Ardhi ya Vijihi, Sura ya 114 (*The Village Land Act, Cap. 114*);
- (xii) Sheria ya Miliki ya Sehemu ya Majengo, Sura ya 416 (*The Unit Titles Act, Cap. 416*); na
- (xiii) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (*The Public Service Act, Cap. 298*).

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, marekebisho ya aina tatu yanapendekezwa. Kwanza, inapendekezwa kifungu cha 128(6) kirekebishwe kwa lengo la kuwaondolea Maofisa Polisi mamlaka ya kufunga mashtaka Mahakamani na kuyahamisha mamlaka hayo kwa Waendesha Mashtaka. Kwa ajili hiyo, maneno “*police officer*” yaliyomo kwenye fungu hilo yanafutwa na maneno “*public prosecutor*” yanaingizwa mahali pake. Maneno hayo yanawajumuisha Maofisa wa Polisi na Mawakili wa Serikali au mtu yejote aliyeteuliwa kuwa Mwendesha Mashtaka.

Pili, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria hii ili kuongeza kifungu kipyga cha 129A kwa lengo la kuwapa Mawakili wa Serikali na Waendesha Mashtaka mamlaka ya kufunga mashtaka mahakamani. Marekebisho hayo yanawiana na yale ya kuhamishia mamlaka ya kufunga mashtaka ya makosa ya jinai kwa Waendesha Mashtaka.

Tatu, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria hii kwa kuongeza kifungu kipyga cha 395A ili kumpatia Waziri mwenye dhamana na mambo ya Sheria mamlaka ya kutunga Kanuni zitakazoweka utaratibu wa namna ya kutunza kumbukumbu za vinasaba vya binadamu zitakazochukuliwa kutoka kwa watuhumiwa wa makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya pili inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara, Sura ya 315. Muswada huu unapendekeza marekebisho yafanyike kwenye Jedwali la Sheria hii ili kuwaondoa wajumbe walio na nyadhifa za Uongozi ama wa Kisiasa au Watumishi wa Umma Waandamizi kuwa mionganoni mwa Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya tatu inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200. Muswada unapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 19 cha Jedwali la Kwanza la Sheria hii ili kuondoa kosa la kupatikana na silaha kinyume cha Sheria kuwa mionganoni mwa makosa ya uhujumu uchumi. Kosa hilo litabaki kwenye Sheria ya *Arms and Ammunition*, Sura ya 223 kwa kuwa adhabu iliyoainishwa kwa kosa hilo ni kubwa kuliko adhabu iliyoainishwa kwa kosa hilo hilo ndani ya Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Nne inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366. Marekebisho haya yanapendekeza kuongeza aya ya (c) katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 42 kinachohusu malipo ya kukatisha ajira (*Severance Pay*). Lengo la mapendekezo haya ni kuwaondoa

watumishi wanaostaafu kutokana na umri, ambao mikataba yao ya utumishi inaisha kutokana na muda wa mkataba katika orodha ya watumishi wanaostahili kulipwa malipo ya kukatisha ajira. Kwa mujibu wa mapendekezo haya, watumishi ambao mikataba yao ya ajira imekoma, watastahili kulipwa mafao ya uezni badala ya malipo ya kukatisha ajira.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya tano inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kurejesha Watuhumiwa Waliofanya Makosa Nje ya Nchi, Sura ya 368. Muswada huu unapendekeza kuongezwa kwa kifungu cha 15A kwa lengo la kuwapatia mamlaka, Mawakili wa Serikali na Waendesha Mashtaka kuiomba Mahakama kutoa amri ya kurejeshwa kwa wahalifu katika nchi walizotendea uhalifu kwa kadiri Mahakama itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya sita inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Inapendekezwa kwamba, kifungu cha 167 cha Sheria hii kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ukiritimba wa Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu kusikiliza mashauri ya ardhi ili mamlaka hayo sasa yatekelezwe na Majaji wote wa Mahakama Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuwapa Majaji wote wa Mahakama Kuu ya Tanzania katika masjala zote nchini, mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ardhi. Ni imani ya Serikali na Mahakama Kuu ya Tanzania kwamba, marekebisho haya yatasaidia kuondoa tatizo la mrundikano wa kesi za ardhi. Hata hivyo, Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu ya Tanzania itaendelea kusikiliza mashauri ya ardhi yanayofunguliwa huko.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya saba inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216. Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanawiana na marekebisho yaliyopendekezwa kufanyika katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na yana lengo la kuipa Mahakama Kuu mamlaka ya kusikiliza kesi za ardhi, tofauti na ilivyo sasa ambapo kesi hizo husikilizwa na Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu pekee. Katika marekebisho haya, kila inapotajwa *High Court (Land Division)* sasa itasomeka “*High Court*”. Kama nilivyoleza marekebisho haya yatapunguza mrundikano wa kesi na hivyo kuwapatia wananchi haki zao kwa wakati. Aidha, inapendekezwa kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 51 kwa lengo la kuainisha maudhui yaliyokusudiwa ili kurahisisha tafsiri, uelewa na utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya nane inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395. Katika Sheria hii, aya ya (c) ya kifungu cha 2(1) inafutwa ili kuruhusu askari polisi kujiunga na kuwa katika orodha ya watumishi wa Mfuko wa Bima ya Afya. Dhamira ya marekebisho haya ni kuruhusu askari polisi kuweza kujiunga na kuwa wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya. Vile vile kifungu cha 6 kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) kwa lengo la kuweka ukomo wa Mtendaji Mkoo wa Mfuko kuwa madarakani. Muda unaopendekezwa ni miaka mitano na kipindi hicho kinawenza kuongezewa kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitano. Sheria kwa hivi sasa haina masharti haya. Pia kifungu kipywa cha 14A kinapendekeza kuweka mazingira yanayoweza kusababisha

kukoma kwa uanachama wa Mfuko. Kwa sasa suala la ukomo wa mwanachama halipo bayana. Kufuatia marekebisho haya, Mwanachama wa Mfuko atakoma kuwa mwanachama endapo atafukuzwa kazi, ataacha kuchangia Mfuko kwa miezi mitatu mfululizo, kama mwanachama akifariki dunia au katika mazingira ambayo Bodi yenewe itaridhika kwamba inafaa kusitisha uanachama wa mwanachama anayehusika.

Muswada unapendekeza pia kufanya marekebisho katika kifungu cha 33 kwa kuongeza aya za (d) na (e) ili kuuwezesha Mfuko kuwekeza katika maeneo yaliyobainishwa katika kifungu hicho. Lengo la mapendekezo haya ni kupanua wigo wa uwekezaji ili Mfuko uwe na uwezo wa sheria wa kuwekeza katika maeneo mengine. Mfuko utakuwa na uwezo wa kuwekeza katika miradi yenye manufaa kwa wanachama na jamii kwa ujumla kwa kuzingatia miongozo (*Guideliness*), itakayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Pamoja na marekebisho hayo, sehemu hii pia inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 37(a) kwa kufuta neno “Board” na badala yake kuweka maneno “*The Controller and Auditor General*”.

Dhamira ya marekebisho haya ni kuondoa mamlaka ya Bodi kuwateua Wakaguzi wa Hesabu ili mamlaka haya sasa yawe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya tisa inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Hati za Kusafiria, Sura ya 42 kwa kuongeza aya mpya ya (g) katika Jedwali la Pili kwa nia ya kuruhusu Mawakili wa Serikali kupewa Hati za Kusafiria za Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kumi inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mbegu, Sura ya 308. Kifungu cha 4 cha Sheria hii kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpatia Waziri Mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Bodi kutoka mionganini mwa watu ambao hawana wadhifa wa kisiasa au sio Watumishi wa Umma Waandamizi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kumi na moja inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Miliki ya Sehemu ya Majengo, Sura ya 416. Kifungu cha 70 cha Sheria hii kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuruhusu Mahakama Kuu kusikiliza kesi zinazohusu migogoro ya ardhi inayoangukia katika sheria hii badala ya Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu. Kama nilivyokwisha kuelezea sababu ni kuwapatia Majaji mamlaka ya kusikiliza mashauri hayo badala ya Majaji wa Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu pekee.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kumi na mbili inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114. Katika Sheria hii inapendekezwa kufanyika marekebisho katika kifungu cha 62 kwa lengo la kuipa Mahakama Kuu uwezo wa kusikiliza kesi za migogoro ya ardhi tofauti na hali ilivyo sasa ambapo kesi hizo zinasikilizwa na Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu pekee.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kumi na tatu ambayo ni ya mwisho kupendekezwa kufanyiwa marekebisheso ni Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Marekebisheso yanayopendekezwa ni kuitia Jedwali la Marekebisheso.

Sehemu mpya ya kumi na nne; dhamira ya marekebisheso haya ni kumpatia Rais mamlaka ya kuteua Katibu wa Sekretarieti ya Ajira. Vile vile inapendekezwa kuweka masharti ya sifa na kipindi cha kutumikia madaraka yao Wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira. Aidha, yapo marekebisheso ya kiuandishi yanayopendekezwa kufanyika katika baadhi ya vifungu vya Sheria ya Utumishi wa Umma ili visomeke vema na kueleweka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kuitia kwako, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika ngazi mbili zinazofuatia ili Bunge lako likiridhia marekebisheso yote yanayopendekezwa yakubaliwe kuwa sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu ninamwita Mwenyekiti wa Kamati atoe maoni ya Kamati.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITU WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, baada ya kukamilisha kazi ya kuuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2009 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Bill, 2009*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 15 Januari, 2010 Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wataalamu mbalimbali wa Serikali. Katika Kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa Muswada huu kwa ujumla wake unapendekeza kuleta marekebisheso ya Sheria Mbalimbali zilizotungwa na Bunge. Kamati ilielezwa kuwa marekebisheso haya yatasaidia utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, katika ufanuzi wa kina uliotolewa na Mheshimiwa Frederick M. Werema, (MB) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilielezwa kuwa, Muswada umegawanyika katika sehemu kumi na nne, ambazo ni pamoja na mapendekezo yanayokusudia kufanya marekebisheso katika Sheria ya Uhujumu Uchumi,

Sura ya 200; Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, Sura ya 366; na Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa.

Sehemu nyingine za Muswada huu zinapendekeza kurekebisha Sheria ya Hati za Kusafiria Sura ya 42; Sheria ya Kudhibiti Viwango vya Mbegu, Sura ya 308; Sheria ya Miliki ya Sehemu ya Majengo, Sura ya 416; na Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unapendekeza kurekebisha Sheria za Kumrejesha Mtuhumiwa Aliyefanya Makosa Nje ya Nchi, Sura ya 368; Chuo cha Elimu ya Biashara, Sura ya 315; na Sheria ya Ardhi, Sura ya 114. Aidha, wakati mtoa hoja alipotoa maelezo ya Serikali kuhusu Muswada huu, aliwasilisha pia Jedwali la Marekebisho kwa lengo la kupendekeza marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilipata fursa ya kuwasikiliza wadau walioalikwa kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Ofisi ya Bunge ilitoa matangazo kwa umma kuhusu tarehe ya kusikiliza maoni ya Wadau juu ya Muswada huu. Tunawashukuru *National Organization for legal Assistance (NOLA)* na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Right Centre*), kwa mchango wao wa kina ulioiwezesha Kamati kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Muswada huu, Wajumbe walitoa hoja mbalimbali na kujibiwa na upande wa Serikali. Wapo waliota angalizo kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa lengo la kuruhusu Mfuko huo kuwekeza katika nyanja zitakazosaidia wateja wake na jamii kwa ujumla. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hoja zote zilizotolewa zilifafanuliwa kwa kina na Mheshimiwa Frederick M. Werema, (MB), Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu utakaosaidia katika maeneo kadhaa ikiwemo utatuvi wa mrundikano wa mashauri kuhusu migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo pamoja na maoni ya ujumla kuhusu Muswada ulio mbele yetu, sasa naomba kutoa Maoni ya Kamati kuhusu maeneo mbalimbali ya Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Muswada huu inarekebisha kifungu cha pili cha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216, ili kuongeza wigo wa Mahakama hiyo kwa kufuta tafsiri ya maneno *High Court (Land Division)*. Kamati inashauri kuwa Ibara ya 19 ifute maneno (*Land Division*) na kuacha maneno *High Court* yaendelee kuwepo katika Kifungu cha pili cha Sheria inayopendekezwa kurekebishwa ili kuendana na Kifungu cha 21 cha Sheria inayorekebishwa (*Principal Act*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya 20 ya Muswada huu inayofuta kifungu cha 51 cha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Kamati ina maoni kuwa Kifungu kipywa cha 51 kinachopendekezwa na Muswada huu kinamruhusu Waziri mwenye

dhamana ya Sheria na Katiba kuandaa Kanuni za utaratibu wa kufuatwa kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) vya Kifungu kipywa cha 51. Kwa kuwa Baraza la Ardhi la Wilaya na Baraza la Nyumba yanayotajwa katika kifungu kipywa cha 51(2) yapo chini ya Waziri mwenye dhamana ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kamati inashauri kuwa kifungu kipywa cha 51(3) kimruhusu Waziri mwenye dhamana ya Masuala ya Katiba na Sheria kuandaa Kanuni kwa madhumuni ya kifungu kipywa cha 51(1) na 51(2), baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofika Ibara ya 24 inayohusu mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 14A cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ilibaini kuwa marekebishesho yanayofanyika yanataja ukomo wa uanachama wa Mfuko wa Bima ya Taifa ya Afya kwa kutolipa michango kwa miezi mitatu mfululizo. Hata hivyo, marekebishesho hayo hayatofautishi kuacha kutoa michango kwa kukusudia na kutotoa michango kwa sababu nyinginezo. Kamati inashauri kuwa, Kifungu kinachorekebishesha kitofautishe namna hizo mbili za kutotoa michango.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine tulilolitolea maoni ni kuhusu rejea ya Sheria zinazopendekezwa kurekebisha sehemu ya kumi na moja ya Muswada wa Sheria ya Marekebishesho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009, inahusu mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Viwango vya Mbegu Sura ya 308 (*The Seeds (Regulation of Standards) Act, Cap. 308*). Hata hivyo Muswada unataja Sheria ya Mbegu (*Seeds Act*) ambayo haipo. Kamati inashauri kuwa, sehemu ya kumi na moja ya Muswada uliopo mbele yetu itaje vyema Sheria husika ambayo ni Sheria ya Kudhibiti Viwango vya Mbegu, Sura ya 308 (*The Seeds (Regulation Standards) Act, Cap. 308*).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hayo ndiyo Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada huu. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuyagusia, Wajumbe wengine wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengine watachangia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebishesho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (*The written Laws (Miscellaneous Amendments), Bill, 2009*). Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Frederick M. Werema, (MB), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Wataalamu wake, kwa ushirikiano na ufanuzi walioutoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Maneno - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Rajab

Hamad Juma, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbiri, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. Aidha, napenda pia kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Elihaika Mtui na Ndugu Athuman Hussein, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu na kuweza kusimama hapa nikiwa mzima na kutoa maoni haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa salamu za heri kwa Watanzania wote ambao wamebahatika kuingia Mwaka huu wa 2010 wakiwa salama na wale waliotangulia mbele ya haki, nawaombea malazi mema peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba kukipongeza chama changu kwa juhudhi za kuleta uelewano na ushirikiano mionganoni mwa Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, Sheria zifuatazo zinafanyiwa marekebisho madogo madogo Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka; Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara; Sheria ya Uhujumu Uchumi; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini; Sheria ya Kumrejesha Mtuhumiwa Aliyefanya Makosa Nje ya Nchi; Sheria ya Ardhi; Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi; Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa; Sheria ya Hati za Kusafiria; Sheria ya Mbegu; Sheria ya Miliki ya Sehemu ya Majengo; Sheria ya Ardhi ya Vijiji; na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazofanyiwa marekebisho ni 13; Kambi ya Upinzani itatoa mapendekezo kwa zile tu ambazo ina wasiwasi kwa vifungu vinavyoongezwa tu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inayorekebisha Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka, kifungu cha nne cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 128 cha sheria. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, marekebisho hayo ni mazuri kwani hilo limekuwa likilalamikiwa na wananchi wengi kwa kuwapa polisi kuwa wao ndio wenye jukumu pekee la kufungua mashtaka. Hivyo, kifungu hiki kitaondoa ukiritimba wa polisi na kwa njia hii tunaamini kuwa, uonevu na mambo mengine yasiyo na msingi katika kadhia nzima ya utoaji wa haki, yatapungua kama si kumalizika. Kambi ya Upinzani inauliza je; Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (*DPP*)

imejiandaa vipi kwa kuwa na watendaji wa kutosha kuziba pengo ambalo litaachwa na polisi?

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 9 ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya. Kifungu cha 23 cha Muswada kinakifanya marekebisho kifungu cha pili cha sheria na kutoa nafasi kwa askari polisi kuwa wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya. Kambi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni busara kwani hata askari wa Jeshi la Ulinzi nao wangeingizwa na kuwa wanachama kwani mahitaji ya watu wote ni sawa na ugonjwa haubagui huyu kaajiriwa na asasi gani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 cha Muswada kinafuta na kurudisha kifungu cha 14A cha Sheria kinachohusu ukomo au usitishwaji wa uanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya. Kifungu kipywa cha 14A (b) kinachosema kuachishwa kazi kwa mwanachama ni ukweli kwamba si wanachama wote amba wanapata huduma hiyo japokuwa wanachangia Mfuko huo kila mwezi. Kama ikitokea kuwa mwanachama hajawahi kupata huduma yoyote ya matibabu na bahati mbaya akaachishwa kazi; je, kuna jinsi ya kupata fidia ya kile alichokuwa anachangia?

Kifungu cha 14A(c) kinazungumzia kushindwa kuchangia mfuko kwa miezi mitatu mfululizo. Kambi ya Upinzani inaona hapa mwanachama atakuwa hajatendewa haki kwa sababu anayeleka mchango ni mwajiri na siyo mwanachama. Je, katika mazingira ambayo mwanachama anakatwa kila mwezi lakini mwajiri hapeleki mchango huo kwa wakati; mwanachama huyo anakuwa *victim of circumstances*? Suala hili linatokea kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na uzembe kama huo unajulikana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa pindi itakapotokea mwanachama akiona hakutendewa haki kwa kufutwa uanachama ni mamlaka ipi anaweza kupeleka malalamiko yake (*Appeal Authority*)?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25(a) cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 33 cha Sheria, kinataka kubadilisha asilimia ya matumizi ya utawala kutoka nane na kuwa kumi na tano kutoka kwenye faida ya Mfuko. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni vigezo gani vimesababisha kupanda kwa hiyo asilimia kwa matumizi ya kiutawala?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Maghimbii. Waheshimiwa Wabunge, kwa Muswada huu ninao wachangiaji watatu; Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Martha Umbulla. Nadhani ni haki tu kusema kwamba, nafasi ipo kwa wale wengine wote ambao wangependa kuchangia kwa sababu tuna muda. Kwa hiyo, kwa mpangilio huo sasa namwita Mheshimiwa Vita Rasid Kawawa, pia ajiandae Mheshimiwa Shellukindo atakayefuata.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill*).

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu, naomba kwa ruhusa yako kwa niaba ya familia ya Marehemu Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa, nikushukuru wewe binafsi na Naibu Spika, Wabunge wote, Wananchi Wote na Viongozi wa ngazi mbalimbali wakiongozwa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kuvisahau vyombo vya habari, kwa kuungana nasi wanafamilia katika majonzi makubwa yaliyotufika sote Wananchi wa Tanzania kwa kuondokewa na Mzee wetu. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu. Naomba nianze kwa Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, sehemu ya 7, vifungu vya 16 na 17 vya Muswada. Napongeza hatua ya kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii, kwani yatasaidia kupunguza mrundikano wa kesi za ardhi mahakamani na gharama zilizokuwa zikitumika kwenda mikoani kwa ajili ya kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yatapunguza pia muda mrefu uliokuwa unatumwi kusikiliza kesi hizo kwa sababu baada ya marekebisho haya, Mahakama Kuu zitakuwa zinasikiliza kesi hizi za ardhi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa, elimu itolewe kwa wadau ili kujuu ni utaratibu gani utakaotumika kwenye kipindi hiki cha mpito kwa kesi ambazo bado ziko Mahakama Kuu (*High Court – Land Division*) kwa sasa hivi na ambazo bado hazijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niende pia sehemu ya 9 ya Muswada huu, kifungu cha 22 mpaka cha 25 kinachozungumzia Mfuko wa Bima ya Afya, Sheria Na. 8 ya Mwaka 1999 ambayo Serikali imeleta mapendekezo ya marekebisho sheria ili Mfuko huu uweze kuingiza Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naunga mkono asilimia mia kwa mia marekebisho hayo ambayo ni muhimu sana na ambayo yamekuja kwa wakati muafaka kuhusu afya za askari wetu na familia zao na vile vile ustawi wa askari hawa mara wanapostaafu kwani inasema kwamba, wanapostaafu pia huduma hizi zitaendelea kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za Mfuko huu kwa wale wastaaafu wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuwajumuisha askari ni wa maana sana, ni utaratibu ambao upo katika nchi nyingi duniani zenyenye uchumi wa wastani kama vile Albania, Sudan na kadhalika. Hivyo, ni utaratibu rahisi unaoendana na utekelezaji wa Sera ya Serikali ya mabadiliko katika Sekta ya Afya. Lakini pia utakuwa unatekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2005, Ibara ya 66(h).

Mheshimiwa Spika, kuna mambo muhimu ya msingi ambayo Mfuko wa Bima ya Afya unapaswa kuzingatia. Naomba nitoe ushauri: Kwa kuwa idara hizi za dola ni muhimu ni taasisi nyeti sana, hivyo hatua za tahadhari zitakazochukuliwa zichukuliwe mapema ikiwemo maandalizi ili kufanya utaratibu uwe wa manufaa yaliyokusudiwa kama elimu ya kutosha kwa kundi hili itolewe lakini waweze kuelewa vizuri haki na wajibu wao na pia waelewe majukumu ya wadau wengine ili kuepusha lawama.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya ihakikishe vituo vya tiba vya majeshi haya vinapata dawa za kutosha kutoka *Medical Stores Department*. Mfuko pia uwe na Kitengo Maalumu au Maafisa Maalumu watakaoweza kusimamia utaratibu mzima wa kufuatilia hadi utakapoimarika. kifungu cha (25) kinabadilisha maana ya awali kuwa maana mpya ambayo itawezesha Mfuko huu kuwezeshwa au kuongezewa uwezo. Naunga mkono majukumu ya Mfuko yameongezeka sana sasa hivi kwa maana hapo awali ulipoanza, ulianza katika maeneo machache lakini sasa hivi uko mpaka vijiji na tumeongezea kundi la maaskari, kwa maana ya vyombo na Taasisi za Dola. Kwa hiyo, kuwezeshwa kwa Mfuko kutoka asilimia nane mpaka kumi na tano mimi naunga mkono ili uweze kutoa huduma yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wanachama wengi wa Mfuko huu wanategemewa na wategemezi wao wako vijiji. Wengi wao wanahitaji huduma muhimu na taarifa, kwa hiyo naomba Mfuko huu pia utoe elimu ya kutosha. Upo utaratibu wa elimu wa Kata kwa Kata lakini hautekelezwi inavyopaswa mwaka hadi mwaka, kwa maana ya kwamba sababu za msingi ni fedha. Kwa hiyo, ninaamini kabisa wakiongezewa asilimia hii Mfuko huu utasaidia utaratibu wa kutoa elimu ya kutosha, uratibu na kusimamia katika vijiji vyetu na kata hadi kata na kuondoa zile lawama katika Mfuko huu au katika Sekta hii ya Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Afya na TAMISEMI wakae na kutoa miongozo ya matumizi ya fedha zinazokusanywa ili ziweze kuonesha matokeo ya thamani ya Mfuko huu. Mfuko wa Afya ya Jamii kule Vijiji na Mfuko wa Bima ya Afya; Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI watoe miongozo ya matumizi ya fedha zitakazokusanywa. Mfuko wa Bima ya Afya pia una jukumu zima la kuhudumia Sekta ya Afya; mojawapo ya jukumu ni kuendeleza miundombinu kwa sababu kazi hiyo ni ya Serikali. Hivyo, katika kifungu cha (25)(d) ambacho kinasema: “*Any investment of the Fund shall be for short or long term investment aimed at improving or enhancing the provision of health services to its members or the general public.*”

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema awali kuwa Mfuko huu wa Bima ya Afya una jukumu zima la kuendeleza huduma za Sekta ya Afya, mojawapo ni kuendeleza miundombinu kwa sababu kazi hiyo ni ya Serikali na kwa kuwa rasilimali za uboreshaji na hizi za afya zinategemea zitokane na fedha zinazochangiwa katika eneo hilo; hivyo kwa kuruhusu Mfuko huu kuwekeza katika vitega uchumi kwa muda mrefu tutauwezesha kumudu vyema na kutoa huduma za kuendeleza miundombinu tiba.

Kwa mfano, kule kwangu Namtumbo tuliomba mkopo katika Mfuko huu kuweza kupatiwa fedha za vifaa tiba na kukarabati wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya Namtumbo; tulishindwa kupata fedha hizi kwa sababu marejesho yake yasingewenza kukidhi sheria, kwa maana marejesho yake yangezidi ile miezi 24 na Sheria ya awali ilikuwa miezi 24 lakini kwa sasa hivi kwa kuwa tutakuwa kwenye *long term*, Sheria itaruhusu zaidi zaidi ya miezi 24 mpaka miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kuwa, Vituo vyetu vya Afya navyo vitawenza kupatiwa fedha za kuweza ku- *invest* katika urekebishaji au ukarabati wa vituo vyetu vya afya na ujenzi wa wodi mbalimbali katika vituo hivyo. Kitu cha msingi kwa Mfuko huu, naomba uzingatie sera yake na uwekezaji pia uendelee kufuata miongozo mbalimbali iliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni huo, naomba kuunga mkono hoja hii.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa. Sasa namwita Mheshimiwa William Shellukindo, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2009. Awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa uwasilishaji wa Muswada huu kwa ufanisi mkubwa sana na hasa ukizingatia kuwa ni mara yake ya kwanza, nadhani tunastahili kumpongeza *sana*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuunga mkono marekebisho yote yaliyoletwa kwa sababu yana shabaha ya kuboresha Sheria hizi ili ziweze kutekelezwa kwa ufanisi. Mimi nitajikita kwenye maeneo yafuatayo: Sehemu ya saba kwenye Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; sehemu ya 8 ya Muswada ya Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216; sehemu ya 12 ya Sheria ya Miliki ya Sehemu ya Majengo, Sura ya 416; na sehemu ya Sheria ya Ardhi za Vijiji, Sura ya 114.

Kwa kweli marekebisho haya ni muhimu sana kwa sababu sasa hivi vijiji vinahangaishwa na mtu mmoja mmoja ambao wanavamia maeneo yaliyoachwa wazi kwa ajili ya shughuli za kijamii na imechukua muda mrefu sana mpaka wananchi wanauliza kwamba kupewa madaraka ya ardhi haya kwenye vijiji kuna maana gani kama migogoro haiishi mapema?

Mheshimiwa Spika, mathalani katika kijiji changu kimoja kinaitwa Kata ya Baga, Tarafa ya Mgwashi, Jimbo la Bumbuli, wana kesi mbili zimewahangaisha zaidi ya miaka mitano na inabidi wasafiri kwenda mpaka Tanga kwenye kesi hizo kutoka kijijini hapo. Kwa hiyo, nadhani hapa kuna haja ya kuangalia vijiji hivi vitasaidiwaje kwenye kesi zao; kwa mfano, katika Wilaya ya Lushoto, Halmashauri ya Wilaya haina Mwanasheria na ninaamini pengine kuna Halmashauri nyingi hazina Wanasheria. Mimi nadhani jukumu hili lingechukuliwa na Wizara ya Sheria, pamoja na *Attorney General*, wapelekwe

Wanasheria wa Serikali kuweza kusaidia kwenye kesi hizi za vijiji. Tukifanya hivyo, tutapunguza matatizo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna baadhi ya kesi imebidi nitafute wakili wa kwenda kusaidia; kwenye kijiji changu kimoja cha Mbuzii, kulikuwa na eneo ambalo lilitolewa zamani na Chifu kwa ajili za huduma za jamii; mtoto wake mmoja ambaye hahusiki na urithi akalivamia ikabidi twende Mahakamani; sasa kesi imechukua muda mrefu ikabidi niwasaidie kuweka Mwanasheria wa kuwasaidia au *Private Advocate*. Nadhani pamoja na uzuri wa kubadilisha Sheria hizi ili tufanye kazi vizuri kuna haja ya kuliangalia suala hili na tusiliachie tu Wizara ya TAMISEMI kwa sababu hii ni kada ni vizuri kuwe na utaratibu wa *allocation* kwamba, hawa wakiteuliwa wakimaliza masomo yao wanakuwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa sababu Halmashauri za Wilaya ni moja ya sehemu ya Serikali ya Tanzania au Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, lile ni tawi tu kwa hiyo katika ugawaji wa wataalamu hawa hapa ni vizuri Serikali ikaliwekea utaratibu suala hili ili kupunguza matatizo ambayo Halmashauri na Vijiji yanapata na yanakatisha tamaa. Wakati kwingine unakuta wanajenga shule, mtu mmoja anakwenda kuchukua *court injunction* kuwa lile eneo ni la kwake kwa hiyo kesi inachukua muda mrefu. Ninaamini Mahakama Kuu inajua wajibu wake, wataweza kuweka msisitizo wa kushughulikia jamii au kijiji kizima kuliko zile za mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo na mimi nilitaka kulichangia vilevile ni hili ambalo limefanyiwa masahihisho na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, ile Sheria ya Mbegu, ambapo yeye amesema ni Sheria ya Kudhibiti Viwango vya Mbegu. Sasa kitu ambacho kimenipa wasiwasi kidogo ni kujua tatizo hasa ni nini; kwa mfano, kusema katika uteuzi wa Mwenyekiti au Mtendaji Mkuu wa Bodi asiwe Mwanasiasa wala Mtendaji Mkuu. Hiyo ya Mtendaji Mkuu nakubaliana nayo kabisa, lakini hii ya Mwanasiasa tuitazame kwa makini; tunazungumza Mwanasiasa kwa namna gani kwa sababu kunaweza kuwa na mtu ni *professional* katika eneo la mbegu, katika eneo la kilimo, lakini ana wadhifa ambao si wa kudumu kwenye chama fulani. Tutatoa mfano, hapa tuna bingwa wa mambo ya kilimo, Mheshimiwa Dkt. Ngasongwa, yeye huenda akawa ana wadhifa wa kisiasa lakini siyo wa kudumu; sasa tuache utaalamu wake huu kwa sababu tu kuna tatizo? Tuelezwe hilo tatizo tuelewe vizuri.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tukiweka *restrictions* ambazo hazisaidii tena kwenye kudhibiti ubora wa mbegu tunataka mbegu hizi zisambae ziende kwa wananchi; kwenye ugani huko sasa kama hawa wanaitwa wanasiasa, wanaambiwa wasisogee kwenye maeneo haya; kuna siri gani hasa tungetaka kujua tatizo ni nini ili na sisi tuweze kulielewa maana tunapitisha Sheria hapa mimi nitaulizwa kwa nini mnataja wanasiasa na wanasiasa hasa ni akina nani? Kwa kiingereza ni ambao wana *political force*. *Political force* hizi ni za namna gani; ni za *executive* au ni za kuhudhuria tu mikutano kwa sababu mtu ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa lakini ni mtaalamu wa mambo yake; ni vizuri pakawekwa wazi hapa ili tusije kupata mgogoro.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono mapendekezo yote pamoja na ile Sheria ya *Public Service* ambayo yameletwa nyuma. Napenda kuyaunga mkono kwa sababu hayapo katika ile *main text*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Martha Umbulla na tutahitimisa na Mheshimiwa Professor Idris Mtulia.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kubaini upungufu katika Sheria zilizoainishwa katika Muswada huu. Hii itaboresha utekelezaji wa Sheria kupunguza adha kwa wananchi walengwa na itawezesha haki kutendeka. Muswada huu umelenga Sheria chache sana kati ya zile tunazodhani zina upungufu mwingi na pengine hata nyingine kuitwa na wakati na ambazo hata Wananchi wamepigia kelele sana. Kwa hiyo, nitaomba katika utangulizi huu kusema kwamba, pengine ni vizuri Serikali au Wizara husika ikaanza kuchambua Sheria nyingi ambazo zina matatizo ili kuweza ku-*harmonise* kulingana na matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi kwa sehemu kubwa ilionekana kunyanya sana wananchi na hasa wanawake. Nimesema hivyo kwa sababu kesi nyingi zinazosikilizwa ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa na pengine Kitengo Maalumu cha Mahakama Kuu ilionekana kuwa na upungufu mkubwa na kuhamasisha rushwa kwa sehemu kubwa na bado katika eneo hilo ilionekana waathirika wakubwa ilikuwa ni wanawake kwa sababu dhahiri kwamba, wanawake hasa wa vijijini hawana fedha za kuhonga zile hongo za aina mbili; ya pesa na ile nyingine. Nina ushahidi wa mama mmoja mjane ambaye alihangaika sana kudai haki yake kwa zaidi ya miaka kumi na kila ngazi alikopita katika hatua hizo za mwanzo alishindwa kesi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri alipokuja kwangu nikamwelekeza kwa wakili mmoja mashuhuri pale Mjini Arusha, Bwana Alute Mgwayi na sijui yeye alitenda miujiza gani kwa sababu ile kesi ilihama kutoka Baraza la Ardhi Babati ikaenda Mahakama Kuu ya Arusha; na kwa sasa nafurahi kutangaza kwamba, alishinda hiyo kesi. Sasa ni dhahiri kwamba, marekebisho ya Sheria katika kupanua wigo wa kusikiliza kesi inaonesha kuwa ina mafanikio na kwa hiyo tunaipongeza Serikali kwa kurekebisha Sheria hii pengine italeta manufaa zaidi kwa wananchi na hususan wanawake.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mwingi tu katika Sheria zetu mbalimbali kama nilivyosema na hasa katika zile Sheria zinazolenga usikilizwaji wa kesi kwenye mahakama za mwanzo hapa nchini. Katika Mahakama zetu rushwa imekithiri sana hasa katika Mahakama ya Mwanzo. Nasema hivyo kwa sababu kesi inachukua muda mrefu sana na niwieni radhi kwa kuwa mimi siyo Mwanasheria nazungumza kwa ujumla tu, lakini kuna tatizo kubwa la usikilizwaji wa kesi katika eneo hili na rushwa ni dhahiri imekithiri kwa sababu watendaji wanachukua rushwa upande wa walalamikaji na walalamikiwa na haki inachelewa kutendeka kwa kuwa kesi inachukua zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo bado waathirika wakubwa ni wale watu wasio na uwezo, wasiojua kusoma na kuandika na zaidi sana wengi wakiwa ni wanawake. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali nayo iangalie upya Sheria inayohusu usikilizwaji wa kesi katika Mahakama zetu za Mwanzo ili vilevile sheria iweke bayana ni hatua gani kali itakayochukuliwa kwa Mahakimu ama wahusika wanaochukua rushwa ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi na haki itendeke mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, ni mara nyingi tumesimama hapa kujaribu kulalamikia Sheria zetu zilizopitwa na wakati hasa zile ambazo ni kandamizi na zinazonyanyasa wanawake. Kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka Serikali imeanza kutambua marekebisho. Tunaiomba pia iweze kuangalia Sheria hizi kandamizi na zile zilizopitwa na wakati ili ziweze kurekebishwa vizuri kulingana na mahitaji.

Mimi sikuwa na mengi ya kuzungumza, nilikuwa na haya machache ya kuchangia katika Muswada huu na ninaunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofî*)

**SPIKA:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, mchangiaji wetu wa mwisho kwenye Muswada huu.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Jaji Werema, kwa jinsi alivyoweza kumudu vizuri kuuelezea Muswada huu hasa ukizingatia kwamba hii ni mara yake ya kwanza. (*Makofî*)

Naomba vilevile niipongeze Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI, kwa kukubali na kuona umuhimu wa Mifuko Afya ya Mikoani na Mawilayani kuunganisha chini ya Mfuko wa Taifa wa Afya na kwamba iwe chini ya uratibu wake. Naomba nijikite katika mabadiliko ya Sheria yanayohusu Mfuko wa Taifa wa Afya. Kwa ujumla ninakubali na kuunga mkono marekebisho mengine yote yaliyoletwa na Muswada huu. Hapa ninaomba kutilia mkazo kwamba, kuwaingiza katika huduma za Mfuko huu wanajeshi wetu; Mapolisi, Magereza na Uhamiaji ni jambo kubwa na la busara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida watakayopata askari ni kubwa, haitakuwa faida kwa askari peke yao bali na jamaa zao wote. Nadhani Sheria hii ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa unakuwa bibi na bwana pamoja na wengine wanen. Kwa hiyo, utakuwa umemsaidia huyu askari afanye kazi vizuri wakati anajua afya yake, ya mkewe na ya watoto wake inaangaliwa vizuri. Kwa hiyo, hoja yangu tangu zamani imekuwa kwa vile tumekubali Mifuko ya Afya ya Jamii ambayo imechukua kila Mtanzania popote aliko iingizwe katika Mfuko huu, ninaomba wigo upanuliwe zaidi ili wananchi wa kawaida na wao waruhusiwe kujiunga na Mfuko huu mradi wanaweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hoja yangu ya kwanza. Katika kipengele cha 25 kuhusu kuuvezesha Mfuko, imetolewa hoja kwamba, Mifuko mingine yote inatumia 15% kwa uendeshaji ila mfuko huu umeruhusiwa kisheria 8%. Hii ni kidogo sana kwa sababu shughuli za Mfuko huu ni kubwa sana na sasa itatanda Tanzania nzima, itahitaji kuelimisha, itahitaji kufungua ofisi nyingi, itahitaji kufuatilia kwa mfano Jiji la Dar es

Salaam ofisi iko Kurasini, kazi nzuri imefanyika pale. Bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa huduma za Jamii na tumekwenda pale tumetazama maendeleo mazuri na kwa kweli hawa jamaa wanapata *Clean Certificate* karibu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa ili iwafikie watu wa Dar es Salaam milioni nne na kitu ni wajibu sasa wa Mfuko huu uzidishiwe fedha ili kufungua matawi mbalimbali kama Zones za Dar es Salaam. Mtu akiwa na tatizo Ubungo kule asisumbuke kwenda Kurasini, kwa hiyo, jambo hili linatia mkazo kwa nini tukubali haraka hawa jamaa wapewe 15% ya mapato yao ili watumie katika Utawala. Hoja yangu nyingine ilikuwa katika kifungu cha 25 vilevile nayo ni kuhusu uwekezaji; Mfuko huu umeanza katika kuwekeza ili kuleta ufanisi katika Afya ya Jamii. Katika Hospitali nyingi wameruhusu mikopo ya vifaa tiba na mimi nataka nitamke hapa kwamba, Hospitali ya Utete Rufiji ilikuwa ya kwanza kupata faida kwa sababu ilipewa mkopo kwa ajili ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanarufiji watumiaji wa hospitali ile, naomba kuushukuru sana Mfuko huu na Waasisi wake walioamua kwamba sasa wanaweza kuleta maendeleo na ufanisi kwa kukopesha hospitali mbalimbali vifaa tiba ili watu wapate huduma nzuri. Isitoshe naomba kusema tena kwamba, wale wa Utete wamesharejesha tayari sasa tunataka tukope tena na kwa kuwa *Amendment* hii inatuwezesha kukopa na kulipa kwa muda wa miaka mitano, jambo hili naona ni zuri sana na ninaomba kuwapongeza na kuipongeza Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, zipo nchi nyingi sana zimetumia vema mifuko hii. Mathalani Nchi ya Korea, hospitali kubwa kuliko zote pale imejengwa na Mifuko ya Bima ya Nchi ile. Naweza nikatoa changamoto hapa kwamba, Mfuko wetu huu uweze kujenga hospitali ya mfano, itakata humo humo wagonjwa wanapokuja kutibiwa na hatuwezi kupata hasara wajenge tu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilikuwa nimelizungumza hata katika kikao chetu cha Kamati za Huduma ya Jamii ni kuomba Mfuko huu sasa ufikirie kujiingiza katika *manufacturing of pharmaceuticals*, yaani utengeneze dawa maana tatizo kubwa la Mfuko huu ni kuwa kila ukienda ukionesha ile kadi unamwona daktari lakini unaambiwa dawa hakuna. Umejitahidi sana Mfuko kwa kufanya *accreditation* ya *Pharmacy* mbalimbali kwamba, kama hospitali haina dawa unaweza kupata dawa katika *Pharmacy* fulani. Hili jambo ni zuri lakini moja kwa moja tujenge *pharmaceutical plant*, yaani tutengeneze wenyewe dawa kama Mfuko au tujiingize katika ubia kwa kununua *shares*. Kwa Mfano, kuna *Tanzania Pharmaceutical Company* ya Arusha ni mali ya Watanzania ile tunaweza kununua hata *shares* 50% tukaweza kupata faida kwa sababu katika biashara ya madawa hakuna hasara.

Mheshimiwa Spika, tutapata faida nyingi lakini lililo kubwa na muhimu ni kwamba, watu wetu watahakikishiwa kwamba, dawa zitapatikana katika hospitali zetu. Nilitaka nirudie *point* hii ya kupanua wigo; sisi Wabunge tungejitahidi na ninataka nitamke, tayari nimeshaandika barua ya kuomba na mimi niwe Mwanachama wa Mfuko huu na ninadhani Viongozi wa Mfuko huu watanikubali. Sina magonjwa makubwa lakini ninataka niwe na uhakika kuwa nikiumwa sitakuwa na haja ya kuuza nyumba

zangu nilale Hospitali ya Agha Khan, huu Mfuko unalipa vizuri vipimo vyote na niwaambie watu wanaovuka umri wa miaka 50 lazima wawe na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, magonjwa ya watu wanaovuka miaka 50 hayatibiwi kwa siku tatu kama vijana, watoto wa shule, wa University au vijana wa *40 years*. Sisi magonjwa yetu Mungu apishie mbali, ukipata ni miezi sita, miaka miwili na wapo watu wameingia hasara kwa kupata magonjwa haya wakauza vitu vyao na magonjwa yenyewe yasipone.

Mathalani una ugonjwa wa figo, inatakiwa kila baada ya wiki, utumie shilingi laki tatu na wewe bado unapenda kula; unauza nyumba ya kwanza, unajua figo zitakuondoa Duniani, watoto unawaachia umaskini. Njia nzuri ni kulipa kabla ili ukipata balaa hilo iwe *stock*, iwe figo au magonjwa ya moyo, utakuwa wewe unatibiwa na mali zako hazitaguswa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninasema nukta hii ya mwisho niwaombe sana Wabunge wote wafuate mfano huu. Mimi nimeomba, sijapata barua ya kukubaliwa lakini nadhani nitakubalika; kwa hiyo, nendeni kule tuwe Wanachama wa Mfuko huu.

Baada ya kusema haya machache, naomba kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu mapema na vilevile naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtulia.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea ombi kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee na nadhani ni vema tu kwa sababu muda bado tunao lakini pia tunazingatia jinsia. Vilevile ye ye ni Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa dakika hii. Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia japokuwa ulikuwa umeshataja mtu wa mwisho kuzungumza. Mimi nitazungumza kwa uchache sana, kwa sababu nina maeneo machache ambayo nadhani ni muhimu niyajadili kwa ufupi kwa sababu malengo mazima ni kujenga na kuweza kusaidiana kuboresha sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nimpongeze Mwanasheria wa Serikali kwa kuleta marekebisho ya sheria hizi kumi na tatu, lakini zaidi nimpongeze kwa hatua yake nzuri ambayo ameifanya hasa katika kifungu cha 29 cha Marekebisho ya Sheria ya Mbegu; ukiangalia kipengele cha 29(a) ambacho Mheshimiwa Shellukindo alihoji kwa nini mnawatoa wanasiasa kuna nini huko; ni muhimu tukaelewa kwamba, Wabunge tumekuwa Wajumbe ama Wakurugenzi katika mashirika mbalimbali ya umma na hali kadhalika kuna baadhi yetu ambao tuna hizi nafasi za Uenyekiti wa Bodi; lakini unapokuja katika suala zima la mgawanyo wa madaraka baina ya Bunge na *Executive Branch*, unapokuwa na Wabunge katika vyombo vy ya kiutendaji vy Serikali wakati huo huo Katiba inasema kwamba Mbunge ndiye anayetakiwa kuisimamia Serikali ama Bunge kama *Institution, ina-play oversight role* ya Serikali.

Sasa tunajiuliza ni kwa namna gani huyu Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi au ni Mkurugenzi katika Bodi za Mashirika yetu ya Umma anaweza *whether* katika *role* yake ya Kamati ya Bunge ama katika *role* ya Bunge kwa ujumla wake akahoji chombo cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameanza na hatua moja nzuri sana kwa hii sheria ya kuzuia Wenyeverti, lakini nadhani tunakoelekeea kama ambavyo CAG amekuwa akipendekeza na mimi naamini CAG amelipendekeza hili kwa sababu yeye anakagua mahesabu kule, anajua ni kwa namna gani sisi wanasiasa tunapokuwa katika hivyo vyombo tunashindwa kutenganisha roho zetu mbili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini baadaye japokuwa yatawaumiza wengi, kuna umuhimu wa kufanyiwa haya marekebisho, wameanza na Mwenyekiti waje na kuzuia Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tupo kwenye Kamati; kuna Wabunge ambao ni Wajumbe wa Bodi anajikuta anashindwa kuhimili, unakuta mna *query* kitu kwa kuwa yeye ni sehemu ya huo mchakato inabidi naye atetee! Sasa hapo kuna hatari na kuna taarifa zinaonesha kwamba, kampuni kubwa ya madini ambayo kuna Wajumbe wawili ni Wabunge, iliua *transfer* kwa kampuni nyingine ya madini ambayo iliisababishia Serikali hasara ya mabilioni; Wabunge wako ndani, Serikali imepata hasara, hakuna umuhimu wao ndani inaonekana wanashindwa kutenganisha nafasi mbili. Kwa hiyo, mimi nadhani kuna umuhimu sana baadaye kwa kadiri tunavyoenda kuhakikisha kwamba kama kweli katiba yetu imeelekeza kila mhimili na nafasi yake; Mahakama nafasi yake; Bunge nafasi yake; na *Executive Branch* nafasi yake.

Sasa inapokuja kwenye masuala ya mashirika yetu, tuhakikishe kwamba hatuna Wabunge ama Wakurugenzi ama Wenyeverti kwa sababu wao sasa wanageuka Watendaji wa Serikali na majukumu yao ya msingi ya kuhakikisha kwamba wao wanaisimamia Serikali itekeleze wajibu wake, yanashindikana na matokeo yake mashirika yetu yanakuwa katika hali mbaya. Tuna mashirika karibu 160 lakini yamekuwa yanakufa na hawa Wabunge wakiwemo ndani kutokana na ukweli kwamba tunashindwa kuondoa tofauti hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni wazo langu la kwanza nikiamini kabisa kwamba, baadaye kwa kuwa imeanzia hatua moja tunaweza tukahakikisha kwamba hawa watu wanatoka huko. Inawezekana kuna maslahi huko, lakini itabidi mvumilie ndiyo kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba kazi zetu zinakwenda vizuri na nchi yetu inasogea.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache nirudi kwenye hoja yangu ya pili ya suala zima la Bima ya Afya; kama ambavyo wengine wameongea, napongeza kwa dhati kwa kujumuisha askari wetu ambao kama wote tunavyojua, wanaishi katika mazingira magumu sana na ninaamini askari wengine pia ukitoa Polisi na wao watakuwa *considered* ili kuweza kuhakikisha kwamba afya zao za msingi zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la umuhimu wa kuhakikisha kwamba hii mifuko yetu ya Bima ya Afya inapanuka; hapa kuna tatizo mmoja ambalo ninaliona mimi hasa kwa uzoefu wangu mdogo niliokuwa nao katika Kamati ya Mashirika ya Umma, nadhani ili kuweza kuboresha hii Mifuko, kuna haja ya kuwa ni *mandatory* kwa watumishi wote ukijumuisha na watumishi wa umma kuhakikisha kwamba wao wanakuwa Wanachama wa Bima ya Afya. Sasa hivi kuna kada fulani ya watumishi amba ni wanachama, lakini unapokuja kwenye haya mashirika yetu ya umma, unakuta kwamba kila shirika lina *policy* yake kuhusiana na suala zima la afya na mashirika mengi kwa kuwa yana fedha unakuta badala ya kuandikisha wafanyakazi wake katika Mfuko wetu wa Bima amba ni wa Kitaifa, ukipanuka unaweza kuchangia kwenye maendeleo kama ambavyo Mifuko ya NSSF na mingine inachangia, wanajirejista katika kampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa unapokuwa na shirika linajirejista katika kampuni binafsi na tunafahamu haya makampuni binafsi ya kimataifa ni *very expensive*, kuna haja kabisa *categorically* hasa ukizingatia hayo mashirika ni yake, kutoa maelekezo kwamba mashirika yote yahakikishe kwamba wafanyakazi wake *including* wale *top Management*, wanajumuishwa katika Mfuko wa Bima ya Afya, kwa sababu kuingia kwa ndiyo kutafanya huo Mfuko uwe mpana na hata hizo huduma ambazo hawa wanadhani wanawenza kuzipata kwenye mashirika ya *insurance* binafsi, wangeweza wakaipata na wakati huo huo tunajikuta shirika letu tunalipanua na vilevile likawezesha kwa namna moja au nyingine kushiriki katika ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru, mimi nilikuwa nataka nichangie kwa uchache hayo. Ninaamini kwamba, Mwanasheria Mkuu baadaye maana mwaka umeshaisha, wakati wa uchaguzi tutaangalia namna gani tunaweza kutenganisha hizi nafasi za kiutawala katika mihimili hii mitatu ili nchi yetu iende mbele na siyo mambo yakae tu kwa sababu kuna *interest* za wanasi. Nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee. Waheshimiwa Wabunge, tumesikia kutoka kwenye *floor* kwa wachangiaji, nina hakika Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo tayari kama mtoa hoja, kwa hiyo nitamwita sasa aweze kuzijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ufanuzi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nitajitahidi lakini pia nikikosea naomba mwongozo wako, kwa sababu mahala hapa siyo pa kawaida na hoja ni nzito. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wanane wamechangia na mmoja amechangia kwa maandishi. Kwanza, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati, kwa uwasilisho wa Muswada wake katika hali ile aliyofanya; anasema kwamba pendekeso la Kamati ile Ibara ya 19 ifute tu maneno yaliyopo kwenye bracket "*Land Division.*" Ukiangalia kwenye *schedule of amendment* ambayo imewasilishwa, tunasema kwamba, *The Principle Act is amended by deleting (a), the definition of the term High Court Land Division and substituting for it the following definition; High Court to mean The High Court of Tanzania established by article 108 of*

*the Constitution of the United Republic of Tanzania.* Kwa hiyo, nafikiri jambo hili limeshughulikiwa kama tulivyoshauriwa kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ukisoma sheria yenyewe utaona kwamba, haitoi tafsiri ya *High Court* na ni kwa maana kwamba, Sheria ilivyokuwa ilikuwa inaanzisha ukiritimba wa *Division* ya Ardhi ya Mahakama Kuu. Kwa hiyo, tunachofanya ni kuondoa ukiritimba huo kwa kufuta maneno *High Court Land Division* na tuna-*define High Court* kwa maana ile. Nafikiri ni suala la *style* pia.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili alichosema ni kwamba, kifungu cha 51(3) katika Muswada kama utakavyoona, kimefanyiwa marekebisho na kwamba kilifutwa. Kifungu hicho ambacho kinatoa mamlaka kwa Waziri wa Sheria kimefutwa na mamlaka hayo yapo kwa Waziri anayehusika na mambo ya Ardhi na tunafikiri kwamba yabaki huko huko.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine la Mwenyekiti wa Kamati linahusu Bima ya Afya na maoni yake ambayo ni mazuri ni kwamba, kwenye Ibara ya 24, ukurasa wa tisa wa Muswada anashauri kwamba, wakati mwanachama wa Mfuko anapokuwa ameshindwa kulipa kwa muda wa miezi mitatu aondolewe, tutafautishe kutokulipa kwa makusudi na kwa bahati mbaya au mambo ambayo yanatokana na mwajiri. Nadhani pendekezo hilo ni sawa sawa na tutaongeza neno *without good cause* ili kama kuna *cause* kwa mwajiri wake basi isiwe sababu ya kumfuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Sheria ya Mbegu, mimi ninavyofahamu ni kwamba, kulikuwa na *revision* ya sheria zetu na sheria hii ilibadilishwa jina, ilikuwa inaitwa *The Seed Regulating and Standards Act*, lakini baada ya kufanya *revision* ya sheria sasa inaitwa *The Seeds Act*. Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na maoni yake mazuri, nafikiri sheria ilivyo inataja vizuri jina la sheria yenyewe, lakini mawazo ni mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa pili alikuwa Mheshimiwa Fatma Maghimbii, Dada yangu kisheria na ameuliza maswali muhimu kwamba, Mkurugenzi wa Mashtaka amejiandaa vipi kukabili suala la kupeleka mashtaka yote kwa Mawakili wa Serikali. Kama inavyofahamika na Bunge limepitisha sheria hapa kwamba, *DPP* anayo mamlaka ya kuwachukua baadhi ya Polisi amba walikuwa wanaendesha mashtaka kuwa bado ni waendesha mashtaka. Pili, tumeajiri vijana wa kutosha kwa kipindi hiki na tutaajiri wengine kila hali ya fedha itakapokuwa nzuri kwa ajili ya kupeleka huduma hizi mpaka *level* ya Wilaya, lakini zipo Wilaya ambako tumeanzia na sasa hivi waendesha mashtaka ni Mawakili wa Serikali ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Askari wa Jeshi la Ulinzi, Magereza na Askari wengine kuwa katika Mfuko wa Bima, nafikiri ni wazo zuri na nafikiri kuna Mheshimiwa Mbunge mwingine amelizungumzia. Napenda kusema kwa ujumla kwamba, Serikali sasa hivi inafanya mchakato wa kuwahuisha hawa wote kwenye Mfuko huu, nafikiri tutakapokuwa tayari tutaleta tena Muswada mwingine ikibidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia kwa mtu anayeachishwa kazi kama ni Mwanachama wa Mfuko wa Bima, nadhani hili kwa Sheria ya sasa siwezi kukupa jibu sasa hivi, lakini kama tutaona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo, tutaleta mabadiliko yanayostahili. Vile vile Mheshimiwa Maghimbii, amezungumzia pia suala la mwanachama wa Mfuko kusitishwa; nafikiri jibu lake nimeshalitoa kwamba tunaweza kuongeza maneno *without good cause*.

Mheshimiwa Spika, nimepata *note* hapa kutoka kwa wataalaam inasema kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina tayari imetoa miongozo ili mashirika yote ya umma yachangie katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Serikali kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali itafuatilia utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ibara ya 25 ambayo ina-*amend* kifungu cha 33, kuna maelezo kwamba tuseme ni kwa nini tunapandisha hizi gharama za matumizi kutoka asilimia nane mpaka asilimia kumi na tano. Nadhani Mheshimiwa Profesa Mtulia amelieleza vizuri sana kwamba, kazi za Bodi hii sasa zinapanuka na kama zinapanuka huwezi kuwa na matumizi yale yale, nafikiri ni *logical* kwamba gharama zitapanda.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa kwa ushauri mzuri kabisa; unaweza kukubaliana na mimi kwamba mtoto wa nyoka ni nyoka na umesikia ushauri alioutoa ni mzuri kabisa na nafikiri Wananchi wa Namtumbo wamekusikia na kwa sababu umetoa ushauri katika mambo hayo basi sisi tutapeleka kwenye Wizara inayohusika. Nadhani hukuwa na tatizo la kuuliza swalii lolote na nakubaliana na wewe kwamba, kuwe na usimamizi mzuri hadi utaratibu utakapoimarika. Huu ni ushauri mzuri kabisa, niliusikia kwa mara ya kwanza mwaka 1964 kuhusu umuhimu wa kushirikisha wananchi katika kufanya mambo yao, wakati huo nikiwa mtoto mdogo lakini niliyasikia maneneo hayo pia kutoka kwa Mzee Rashid Mfaume Kawawa. (*Makofi*)

Namshukuru sana Mheshimiwa William Shellukindo, unapopewa ponezei na mtu ambaye amekuwa kwenye Utumishi wa Umma zaidi ya miaka arobaini ni faraja; nashukuru sana. Nafikiri tatizo la uvamizi wa ardhi katika vijiji au suala la vurugu katika mambo ya ardhi pengine limetokana na mfumo wetu wa sheria au limetokana na utamaduni wetu au limetokana na kutofahamu mamlaka au kutofahamu utaratibu na kutoheshimu haki za watu wengine. Hili suala la vijiji kusaidiwa kesi zao nadhani ni pendekezo zuri, tutaangalia uwezekano wa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria, kwa sababu na sisi pia tunabanwa na sheria; unaweza kwenda mahala fulani ukaambiwa huna kiti cha kukaa kwa sababu siyo nafasi ya Wakili wa Serikali. Tutaliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Mbegu, nafikiri suala la Wajumbe wa Bodi ni vizuri tusi-*dramatize*, kitu kinachozungumzwa hapa ni kwamba yule Mwenyekiti asiwe mtu anayeshikilia nafasi ya Uongozi wa Kisiasa au Afisa wa Serikali Mwandamizi lakini Wajumbe wengine bado wanaweza kuwa ni wanasiasa, kama alivyosema Dada yangu wa Kisheria, Mheshimiwa Mdee, nadhani usimwangalie Mdee ila angalia anachokisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakuwa vigumu sana, kwa mfan, kama shirika lina shida na Wabunge wamo, lakini vile vile ni vigumu sana kufanya *separation of powers* ikawa *perfect*. Hakuna mahali popote duniani hata kule Marekani ambako kuna *very perfect separation of powers*, kuna mahali fulani mnaingiliana; kwa mfano, kule Marekani Wabunge wa *Senate* wanawapigia kura Majaji na Majaji wanaomba kura kutoka kwa watu, sisi hapa hatuna hiyo; sasa hiyo *separation of powers* naona ina matatizo kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hapa Rais anawateua Majaji lakini yupo kwenye *Executive*, kwa hiyo, hatuwezi kuwa na *perfect separation of powers*, lakini ni suala ambalo pengine tunaweza kulizungumza, ila kwenye suala la *accountability* pengine ni vizuri tu-draw a line ambako Waheshimiwa Wabunge mtatekeleza kazi zenu za kutunga sheria na kuisimamia Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pendekezo ni kwamba, Mwenyekiti wa Bodi asiwe Mwanasiasa ila mnaweza kukaa kwenye Bodi na yule mtu ambaye ni Profesa yupo Bungeni anaweza kuwa bado Mjumbe wa Bodi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Martha Umbulla, kwa suala lake linalohusu sheria zinazopitwa na wakati. Uzee siyo kashfa na baadhi ya sheria hizi ingawa zimezeeka, lakini ziliandikwa kwa njia ambayo kuisha kwake itakuwa vigumu, lakini kila inapowezekana kutokana na mahitaji sheria hizo zinabadilishwa.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika na ninatumia nafasi hii kuwaomba Watumishi na Bodi za Ardhi zinazoamua mashauri ya ardhi, kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria. Rushwa ambayo inalalamikiwa si ya kubuni ipo na nafikiri tumeshapiga kelele sana kuhusiana na suala hili, sasa nafikiri vyombo vinavyohusika visirudi nyuma kuwashughulikia kwani rushwa inapotosha haki na vitabu vyote vya dini vimeandika hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mwenendo wa mashauri katika Mahakama za Mwanzo na sheria kandamizi ambazo Mheshimiwa Umbulla anazizungumzia, tunaomba kama kuna mapendekezo yoyote basi yaletwe haraka kusudi tuyashughulikie, pamoja na mchakato wa kubadilisha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai ambayo sasa hivi yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Mtulia amezungumzia kwamba wigo upanuliwe ili na askari wengine wahanishwe. Kama nilivyosema na *note* nimeisoma. Ongezeko la matumizi kutoka asilimia nane hadi kumi na tano, nakushukuru sana na kwamba Mfuko utengeneze dawa; nafikiri hilo ni suala la sera litashughulikiwa. Pia nakushukuru sana kutoa elimu nzuri ya uhamasishaji. Bado watu hawafahamu umuhimu wa Mifuko hii ya Bima na kujiwekea Bima.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na tiketi ya ndege unatakiwa kabla hujaingia kwenye ndege hiyo uwe umekata bima yako, kwa sababu ndege inaweza kuanguka na

wewe ukaacha watoto wanapata shida. Unapokuja Dodoma hapa unatakiwa uweke Bima ili ikusaidie kama litatokea jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwaje kama inafika mwisho hujapata janga lolote; je, urudishiwe Bima? Kwa kweli huo siyo utaratibu, suala zima la Bima ni mkusanyiko wa fedha; kuna wengine watatumia kuna wengine hawatatumia na katika nchi nyingine ndiyo mwanzo wa pesa za ku-*invest*. Kwa hiyo, nafikiri na sisi tukichangamkia hiyo tutatatua baadhi ya matatizo yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, ametoa mchango wake kwa maandishi na amekazia sana suala la rushwa na suala la utendaji wa haki kuhusiana na masuala ya kesi za ardhi; mengi ilikuwa ni ushauri na tutauzingatia.

Mheshimiwa Halima Mdee, amezungumzia kuhusu suala la Wabunge kutokuwa kwenye hizi Bodi, nakubaliana naye lakini kwa leo tunaomba yule Mwenyekiti asiwe Mbunge lakini Wabunge wanaweza kuwa Wanachama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani hayo ndiyo mambo makubwa yaliyozungumzwa, naomba sasa niishie hapo. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nilikuwa bado sijamaliza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ukishatoa hoja inatosha. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa mujibu wa Kanuni ya 88 tutaingia katika hatua inayofuata ya kuitisha Muswada.

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)  
**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Act, 2009)**

Kifungu cha 1  
Kifungu cha 2  
Kifungu cha 3  
Kifungu cha 4

Kifungu cha 5  
Kifungu cha 6  
Kifungu cha 7  
Kifungu cha 8  
Kifungu cha 9  
Kifungu cha 10  
Kifungu cha 11  
Kifungu cha 12  
Kifungu cha 13  
Kifungu cha 14  
Kifungu cha 15  
Kifungu cha 16  
Kifungu cha 17  
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19  
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 23  
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25  
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 27  
Kifungu cha 28  
Kifungu cha 29  
Kifungu cha 30  
Kifungu cha 31  
Kifungu cha 32  
Kifungu cha 33  
Kifungu cha 34  
Kifungu cha 35  
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 14

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 37  
Kifungu cha 38  
Kifungu cha 39  
Kifungu cha 40

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko*

*yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Act, 2009)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2009 (*The Written Laws (Miscenelleous*

*Amendments) No. 3 Act, 2009), kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa 2009 kama ulivyorekebishwa sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara  
ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Muswada huo Kusomwa Mara ya Tatu, sasa ni kuthibitisha kwamba Muswada huo wa *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3* wa Mwaka 2009, umepitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa utakwenda katika hatua zinazopaswa hadi kumfikia Mheshimiwa Rais. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizopangwa leo zimekwisha na bahati mbaya Muswada unaofuata ulikuwa bado kuna mambo machache ya kukamilishwa ndani ya Kamati inayohusika, kwa hiyo isingewezekana kuwekwa hata katika *Supplementary Order Paper* kwa sababu haujakamilika. Kabla sijaahirisha Bunge, nitoe tangazo kwamba, Mwenyekiti wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, ambaye ni Waziri Mkuu, anaomba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa kumi na moja na nusu leo jioni.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo langu la saa saba na nusu linabaki pale pale; Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi itakutana saa saba na nusu Ukumbi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo na kwa kuwa hakuna shughuli nydingine tena, naahirisha shughuli za Bunge hadi hapo kesho asubuhi saa tatu.

*(Saa 06.36 mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 29 Januari 2010 Saa Tatu Asubuhi)*